**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**KITIVO CHA SANAA**

**IDARA YA KISWAHILI**

# SAJILI YA MAAFISA WA POLISI: TATHMINI YA MATUMIZI YA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA KITUO CHA POLISI CHA CENTRAL, NAIROBI

**NA**

**RUTH MORAA BINYANYA**

**C50/77931/2012**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.**

**2014**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa popote kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

Sahihi……………………………………………….…Tarehe………………..…………………..

**Ruth Moraa Binyanya.**

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

Sahihi……………………………………….……….Tarehe…………………………………

**Prof. Kithaka wa Mberia**

(Msimamizi)

Sahihi…………………………………….……………..Tarehe…………………...…………

**Dkt. Nyachae Michira**

(Msimamizi)

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu Bw. Naftal Memba Binyanya na Bi. Margret Obonyo Binyanya.Walinifungulia mlango wa elimu kwa kujinyima ili kunielimisha hadi kiwango hiki cha uzamili. Mola awape maisha marefu.

Nawatabarukia, Muhibu wangu Evans, ndugu, kaka na dada zangu kwa kunipa moyo na msaada niliohitaji. Asante kwa mchango wenu; pengine, ningezidiwa na changamoto zilizonikabili. Mungu awabariki.

## SHUKRANI

Safari ya kukamilisha tasnifu hii ilikuwa na pandashuka si haba, lakini nashukuru kwa ushauri, maelekezo na mawazo ya watu kadhaa. Mchango wao mkubwa ulipunguza uzito wa kazi hii.
Natoa shukrani zangu kwa Maulana kwa kunipa afya, nguvu na neema katika kipindi hiki cha shahada ya uzamili na kuniwezesha kuikamilisha. Namshukuru kwa kuwa si lazima kwamba ukianza jambo utalimaliza; wengi huanza safari ila hawafiki.

Shukrani nyingi ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Kithaka wa Mberia na Dkt. Nyachae Michira. Walijitolea kwa hali na mali kunielekeza kila nilipowahitaji. Nashukuru kwa kuwa walikuwa na shughuli nyingi ila waliweza kunihudumia. Nawashukuru kwa mawaidha, tahakiki na maelekezo ya kitaaluma ambayo yalinifaa si haba. Mchango wenu unanifanya kuwa mdeni wenu. Mungu awaongezee hekima.

Nawashukuru wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili kwa ushauri wao na maelekezo yao katika kipindi cha usomi wangu katika Chuo Kikuu cha Nairobi tangu shahada ya kwanza hadi uzamili. Nawashukuru wahadhiri wote walionifunza shahada ya kwanza kwa kunipa motisha ya kujiunga na uzamili. Shukrani zangu ziwaendee Dkt. Mbuthia, Dkt. Mukhwana, Dkt. Swaleh, Dkt. Timammy, Dkt. Omboga, Dkt. Iribemwangi na Dkt. Mweri ambao walinipa msingi mzuri wakati wa shahada yangu ya kwanza. Nawashukuru pia Prof. Habwe na Prof. Wa Mutiso.

Tasnifu hii haingekamilika bila mchango wa maafisa wa polisi wafuatao: Inspekta Mogeni na maafisa wa polisi: Michael na Omariba. Changamoto kubwa ilikuwa namna ya kukusanya data

lakini kutokana na kujitolea kwao tulifaulu. Shukrani nyingi pia kwa Bw. Rithaa aliyechukua muda wake kutuongoza wakati wa kukusanya data.

Safari hii tuliabiri pamoja na wanafunzi wenzangu ambao tulihimizana na kutiana moyo. Naomba Mola aongoze darubini zenu. Mola awabariki Jane, Magdalene, Vincent, Nyangeri, Jael, Sr. Teresia, Regina, Furaha, Mariam, Duncan, Tsuma, Kisakwah, Mwangi, Muthoni, Margret, Schola, Doris na Grace.

Nawashukuru ndugu na mawifi zangu, Joshua, Micah, Simon, Obed, Risper, Tabitha, Esther, Caro, Wangari na Vera kwa kunihimiza na kuniombea dua.

Nawashukuru rafiki zangu ambao siwezi kuwataja wote ila baadhi: Lynne, Seraphine,
Zac, Joash, Stella, Hosea, Hildah na Maryann tuliyehimizana kujiunga na uzamili baada ya shahada ya kwanza. Asanteni kwa kunihimiza na kunipa msaada niliohitaji kutoka kwenu.

Nawashukuru walimu wenzangu wa shule ya upili ya God-Agulu hasa mwalimu mkuu na naibu mwalimu mkuu kwa kunipa ruhusa ya kutoka shuleni kwenda kukusanya data mjini Nairobi. Mwalimu mkuu Bw. Justus Ojuok na naibu wake Bw. Tom Ogola nashukuru kwa mchango wenu.

Watu ambao ningependa kuwashukuru kwa kuwataja majina ni wengi lakini muda na nafasi haitoshi. Pokeeni shukrani zangu hata kama sikuwataja.

**IKISIRI**

Utafiti huu ulilenga kubainisha sajili ya maafisa wa polisi kwa kujikita katika lugha ya Kiswahili. Kazi yetu imepangiliwa katika sura tano ambapo sura ya kwanza tumeangazia utangulizi, sura ya pili tumeshughulikia dhana tunazotumia katika utafiti, sura ya tatu tumeonyesha na kubainisha data kwa mujibu wa nadharia yaBernstein ya misimbo na nadharia ya Giles ya maafikiano ambapo tumeangazia mazungumzo baina ya maafisa wa polisi wenyewe. Sura ya nne tumeonyesha na kuchanganua data kwa mujibu wa nadharia ya vitendo usemi kama ilivyoelezwa na Austin na Searle kwa kujikita katika mazungumzo baina ya maafisa wa polisi na wateja wao.

Mazungumzo baina ya maafisa wa polisi yamedhihirisha matumizi ya msimbo pana wanapozungumzia mambo ya kijumla kama vile siasa na elimu na matumizi ya msimbo finyu wanapozungumzia mambo ya usalama. Tumebainisha kuwa pana maafikiano baina ya maafisa wa polisi kama kikundi cha kijamii kutokana na matumizi yao ya lugha. Mazungumzo baina ya maafisa wa polisi na wateja wao yamedhihirisha kutokea kwa vitendo usemi ambavyo vinadhihirisha athari ya sajili ya maafisa wa polisi. Usemi wa maafisa wa polisi umedhihirisha vitendo usemi ambavyo huwa na sifa ya kutambulika kutokana na kinachosemwa na kani ya ilokusheni. Ili kutaka kujua athari ya kitendo fulani, sharti kuangalia kinachosemwa, kinasemwa wapi, na nani na kwa nani.

## YALIYOMO

UNGAMO .......... ii

TABARUKU .......... iii

SHUKRANI .......... iv

IKISIRI .......... vi

YALIYOMO .......... vii

**SURA YA KWANZA .......... 1**

**SAJILI YA MAAFISA WA POLISI .......... 1**

1.0 UTANGULIZI .......... 1

1.1 USULI WA MADA YA UTAFITI .......... 1

1.2 TATIZO LA UTAFITI .......... 5

1.3 MALENGO YA UTAFITI .......... 7

1.4 NADHARIA TETE ZA UTAFITI .......... 7

1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA .......... 8

1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI HUU .......... 9

1.7.0 NADHARIA .......... 10

1.7.1 NADHARIA YA BERNSTEIN .......... 11

1.7.2 NADHARIA YA MAAFIKIANO .......... 13

1.7.3 NADHARIA YA VITENDO USEMI .......... 16

1.8 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA .......... 19

1.9 MBINU ZA UTAFITI .......... 23

1.9.1 WALENGWA .......... 24

1.9.2 SAMPULI KIELELEZO .......... 24

Jedwali 1.1 .......... 24
1.9.3 MBINU ZA UKUSANYAJI DATA .......... 25
**SURA YA PILI.......... 26**
**DHANA MUHIMU ZA SAJILI YA MAAFISA WA POLISI .......... 26**
2.0 UTANGULIZI .......... 26
2.1 DHANA YA ISIMUJAMII .......... 26
2.2 DHANA YA JAMII.......... 30
2.3 DHANA YA SAJILI .......... 31
2.3.1 MIFANO YA SAJILI .......... 36
2.4 LUGHA YA KISWAHILI.......... 41
**SURA YA TATU.......... 45**
**MISIMBO NA MAAFIKIANO KATIKA SAJILI YA MAAFISA WA POLISI.......... 45**
3.0 UTANGULIZI .......... 45
3.1.1.0 MSIMBO PANA .......... 46
3.1.1.1 KUTOA HISIA.......... 47
3.1.1.2 RAI.......... 49
3.1.2.0 MSIMBO FINYU .......... 50
3.1.2.1 UFAHAMU WA AWALI .......... 50
3.1.2.2 SIRI .......... 51
MAAFIKIANO KATIKA SAJILI YA MAAFISA WA POLISI.......... 54
3.2.0 UTANGULIZI .......... 54
3.2.1.0 KUCHANGANYA NDIMI .......... 55
3.2.1.1 KUJIELEZA VIZURI.......... 56

3.2.1.2 KUFIDIA MSAMIATI ........ 57
3.2.1.3 KURAHISISHA MAWASILIANO ........ 60
3.2.1.4 MSISITIZO ........ 61
3.3.0 SARUFI ........ 63
3.4.0 KUKATIZIANA USEMI ........ 64
3.4.1 KUJIELEZA ........ 64
3.4.2 KUBADILI MADA ........ 65
3.4.3 UREJESHI ........ 67
**SURA YA NNE ........ 70**
**VITENDO USEMI KATIKA SAJILI YA MAAFISA WA POLISI........ 70**
4.0 UTANGULIZI ........ 70
4.1 NADHARIA YA VITENDO USEMI ........ 70
4.1.1 KUTOA AMRI ........ 72
4.1.2 KUTOA ONYO ........ 72
4.1.3 KUVUTA NATHARI........ 74
4.2.0 MATUMIZI YA MASWALI ........ 75
4.2.1 UCHUNGUZI........ 75
4.2.2 KUHIMIZA MAZUNGUMZO ........ 77
4.2.3 UREJESHI ........ 78
4.3.0 NIA YA MZUNGUMZAJI ........ 78
**SURA YA TANO ........ 83**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 83**
5.0 UTANGULIZI ........ 83

5.1 MUHTASARI........................................................................................................... 83

5.2 HITIMISHO............................................................................................................. 84

5.3 CHANGAMOTO ZA UTAFITI................................................................................. 85

5.4 MAPENDEKEZO ..................................................................................................... 86

**MAREJELEO. ........................................................................................................ 87**

**DATA YA UCHANGANUZI........................................................................................ i**

# SURA YA KWANZA

# SAJILI YA MAAFISA WA POLISI

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti huu unahusu sajili ya maafisa wa polisi. Tumejikita katika mtazamo wa Isimujamii ili kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi ambayo huweza kutumiwa kuwatambulisha. Utafiti huu umekitwa katika muktadha mahsusi. Muktadha wa mazingira ya kazi. Hii imetuwezesha kuchunguza hali zinazosababisha uzungumzaji wa namna fulani, matumizi ya lugha na mtindo wao wa kuzungumza.

Mtafiti ametumia mitazamo kadha ili kuweza kuchunguza na kuchanganua sajili ya maafisa wa polisi: tumetumia nadharia ya Bernstein ya misimbo, nadharia ya maafikiano na nadharia ya vitendo usemi. Jambo la msingi katika utafiti huu ni kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi ili kuweza kuichanganua na kuieleza.

## 1.1 USULI WA MADA YA UTAFITI

Lugha haiwezi kupuuzwa wala kudhalilishwa katika jamii yoyote ile. Lugha imeweza kutumiwa kuleta mabadiliko na huwa na athari chanya na hasi katika jamii kutegemea na watumizi lugha: msemaji na msemewa. Katika athari chanya, lugha yaweza kutumiwa kuwaunganisha watu na pia kukomesha uhasama. Hata hivyo, lugha yaweza kuwa na athari hasi hasa ikiwa itatumiwa kuleta uhasama au kusababisha utengano baina ya mtu na mtu, jamii na jamii nyingine au hata makundi ya kijamii. Lugha huweza kuathiri mtazamo na tabia ya mtu. Yote hutegemea namna lugha inatumiwa ili kuleta athari inayokusudiwa.

Watu hutambua kikundi chao cha kijamii kutegemea misimbo au aina ya lugha wanayotumia. Matumizi ya lugha kwa njia fulani ndio huwafungamanisha watu wa kikundi fulani pamoja na kuwatambulisha. Lugha ya maafisa wa polisi huweza pia kubainishwa na kutumiwa kuwatambulisha.

Maafisa wa polisi ndio kiungo muhimu katika kulinda na kudumisha usalama wa nchi. Kutokana na uhalisi wa kazi yao, maafisa wa polisi huhusiana na watu wa matabaka mbalimbali na walio na vyeo tofautitofauti katika nyanja mbalimbali. Katika kutekeleza majukumu yao, maafisa wa polisi hutumia lugha kuwasiliana na 'wateja' wao.

Maafisa wa polisi hutumia lugha kwa namna inayowatambulisha wao kama kikundi maalum ambacho kinaweza kutambuliwa kutokana na sajili yao. Kikundi hiki cha maafisa wa polisi kinaweza kutambuliwa na watu wengine kutokana na lugha wanayoitumia. Kama wasemavyo Linda na Wareing,(1999: 143), kikundi fulani hutambuliwa kama kikundi cha kijamii na watu wengine kutokana na matumizi yao ya lugha na tabia zingine za kiisimu kama vile katika kutunga sentensi zao. Haya ndio mambo ambayo huwaongoza wanajamii wengine kukitambua kikundi cha kijamii. Matumizi ya lugha ya maafisa wa polisi ni ya kipekee na hii huwatofautisha na makundi mengine.

Lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kikundi chochote kile huwa na namna yao ya pekee ya kutumia lugha na hii hutofautisha kikundi na kingine. Habwe na wengine (2010: 71) wanasema kuwa "…………ili kukidhi haja ya

mawasiliano, makundi ya kijamii huibua mitindo na istilahi zao zinazowawezesha kurejelea shughuli za kundi husika."

Hii inaashiria kuwa kila kikundi katika nyanja mbalimbali huwa na mtindo wake wa kutumia lugha kwa namna ambayo itawawezesha kuafikia malengo yao ya kazi. Maafisa wa polisi kama kikundi cha kijamii pia huwa na mitindo na istilahi zao ambazo huwawezesha kutekeleza majukumu yao. Kwa sababu hii, tunachunguza sajili ya maafisa wa polisi ili kubaini lugha yao.
Kwa mujibu wa Fishman (1968: 3) jamii ni ya muhimu kuliko lugha na kwa hivyo anasema kuwa jamii ndio hutuwezesha kupata muktadha ambao unaweza kutusaidia katika kutazama aina ya lugha inayotumiwa. Kwa sababu hii, tumetilia maanani kikundi hiki cha maafisa wa polisi ambacho kinaweza kutambuliwa kutokana na sajili yao hasa matumizi yao ya lugha ya kiswahili.

Tumechunguza sajili ya maafisa wa polisi wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao katika mazingira wanapotekeleza shughuli zao. Kama asemavyo Bernstein (1971: 61) tofauti za kiisimu za matumizi ya lugha ya kikundi fulani hutokea katika mazingira halisi ya kijamii na vyeo vya makundi mbalimbali huweza kubainishwa na usemi wao. Ni rahisi kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi wanapokuwa katika kituo cha polisi kwa kuwa hayo ndio mazingira yanayowatambulisha na ndio muktadha wao halisi.

Fishman (1968: 139) akimnukuu Halliday: uchunguzi wa muktadha wa mazungumzo hutuelekeza katika uchanganuzi wa hali na matumizi ya lugha. Kutokana na ukweli huu, tumechunguza na kuchanganua sajili ya maafisa wa polisi ambayo huwezesha kikundi hicho kutambuliwa, kwa kujikita katika kituo cha polisi cha Central, Nairobi.

Pride (1971: 25) anasema kuwa, mawanda ya matumizi ya lugha huelezwa kama hali ambapo matumizi ya aina fulani ya lugha hutumiwa na kikundi mahsusi na hii husaidia katika utambulisho wa kikundi hicho cha kiisimu na kwa njia ya kijamii. Hii inaashiria kuwa kikundi fulani cha watu huweza kuainishwa kijamii na kiisimu. Kwa kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi, tutakuwa tukichunguza kikundi cha kiisimu na kijamii.

Naye Hirst (1986) anasema kuwa namna watu hutumia lugha husababishwa na mambo mawili: wao kama watu binafsi au wao kama wanajamii. Hii ina maana kuwa, lugha wanayotumia katika mazungumzo huchangia katika kujitambua na pia lugha yao ni chombo cha kudhihirisha kikundi hicho husika.'(TY).

Maafisa wa polisi huwa jamii. Lugha wanayoitumia hudhihirisha kikundi cha maafisa wa polisi. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, ni wazi kuwa kila kikundi katika nyanja mbalimbali huwa na namna yao ya kuwasiliana. Hii huwatambulisha watu wa kikundi hicho.Muundo wa kitabaka huathiri elimu na kazi za watu na kisha kuwapa wanajamii husika mahusiano fulani ambayo hutambulisha tabaka lao ambalo huwa tofauti na matabaka mengine. Ni kutokana na ukweli huu, ndiposa tunachunguza sajili ya maafisa wa polisi.

Kikundi hiki cha maafisa wa polisi ni cha kijamii, na jamii hutumia lugha ambayo hutumiwa kuitambulisha. Wanajamii katika kikundi fulani hutumia lugha kwa njia ya kipekee wanapoingiliana ili kutambuliwa katika kikundi hicho. Hii inadhihirisha kwamba unaweza kuzungumza kama wanakikundi hicho na hivyo kuwa mwanakikundi.

Nchini Kenya kuna chukulizi kuwa lugha ya maafisa wa polisi husheheni kuchanganya ndimi, sauti yao hudhihirisha mamlaka, wana misimbo yao ambayo huitumia katika mawasiliano. Chukulizi hizi ndizo zinazotuchochea kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi. Hata hivyo, tumechanganua data kulingana na nadharia tunazotumia.

Maafisa wa polisi huwa na msimbo ambao wanauelewa wao binafsi. Msimbo wao ni finyu na hivyo hutenga makundi mengine katika uzungumzaji wao. Msimbo ni sehemu ya lugha na ni utaratibu wa kutoa mawasiliano (Iribemwangi na Mukhwana, 2011: 45). Wanaendelea kusema kuwa:

> Kwenye msimbo finyu, wazungumzaji huweza kutumia ujuzi na tajriba zao za pamoja na uelewa wa pamoja kusemea kile wanachotaka kuongea au kusema. Aina hii ya msimbo huunda upamoja ambao hufanya watu wanaotumia lugha kuhisi kuwa ni wa kundi fulani moja.

Kama mkakati wa mawasiliano, maafisa wa polisi hutumia msimbo finyu kama njia ya kuonyesha umoja na kutenga makundi mengine hasa wanapozungumzia masuala yanayohusu usalama wa nchi. Pia hutumia msimbo pana wanapowasiliana na wateja wao. Kwa mfano, msimbo hutumika sana pale wanapozungumza kwa kutumia redio zao za mkononi (*walkie talkie*).

### 1.2TATIZO LA UTAFITI

Mawasiliano ni muhimu kwa maafisa wa polisi wanapotangamana na watu wa matabaka mbalimbali wakati wa utekelezaji wa majukuumu yao. Katika mawasiliano haya, lugha ni

muhimu na isipotumika kwa namna inayoeleweka kati yao na jamii basi kutakuwepo na utata, hivyo hawataweza kuafikia malengo yao ya kuzuia uhalifu.

Lugha ya maafisa wa polisi ina athari fulani katika jamii lakini katika somasoma zangu sijakumbana na utafiti wa kina kama ilivyo tafiti za makundi mengine kama vile wahubiri, wanasiasa na wachuuzi. Kutokana na kuenea kwa athari za lugha ya maafisa wa polisi katika jamii, tumefanya utafiti ili kuweza kuieleza na kuichanganua sajili yao.

Uhusiano na dhamira ni baadhi ya viamuzi vya lugha. Uhusiano wa Maafisa wa polisi na watu wanaokutana nao waweza kuwa wa karibu au wa mbali yaani hawajawahi kukutana hapo awali. Kwa hivyo wanatumia lugha kwa namna mahsusi kutegemea na nani anazungumza na anazungumza na nani. Utafiti huu umekitwa katika muktadha wa sajili ya maafisa wa polisi. Kama asemavyo Bailey (2004) katika makala yake kuwa: Lugha kama ilivyo vitendo, huhakikisha kuwa namna fulani ya kuzungumza na kutenda vimedumishwa na hii ndio huthibitisha uthabiti wa mfumo wa kijamii.

Namna maafisa wa polisi wanavyowasiliana wao kwa wao, au wao kwa wananchi, ni tofauti na watu wa makundi mengine ya kijamii. Dhamira ya maafisa wa polisi ni kuwa hatimaye sheria inatekelezwa. Maafisa wa polisi hawana nia ya kutumia lugha ya kushawishi kama wanasiasa. Lugha ya maafisa wa polisi kwa mfano inatofautiana na ya wahubiri kanisani, kwani wahubiri huwa na lengo la kuongoa roho na kuwapa moyo wanaokata tamaa, kama asemavyo King'ati, (2002: 3) wahubiri hawana budi kuzingatia namna wanavyozungumza ili waumini waweze kudumisha nathari yao. Kwa upande wa maafisa wa polisi, hawana haja ya kuwapa watu

matumaini bali jukumu lao ni kulinda sheria za nchi, na kwa kufanya hivi wao hutumia lugha itakayowawezesha kuafikia malengo yao.

Katika utafiti huu tunachunguza na kuchanganua mambo yanayohusiana na sajili ya maafisa wa polisi. Matumizi haya ya lugha ya maafisa wa polisi yana athari fulani katika jamii lakini katika somasoma zangu sijaweza kupata utafiti wa kina kuwahusu. Pia,haijaeleweka kinagaubaga kinachowalazimu wao kuitumia lugha vile. Huu utafiti utaongezea kiwango cha yaliyoandikwa kuhusu mada kama hizi.

## 1.3 MALENGO YA UTAFITI

Katika utafiti huu wa kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi kwa kujikita katika lugha ya Kiswahili, tuliongozwa na malengo fulani. Malengo hayo yanatuwekea msingi wa kubainisha sajili ya maafisa wa polisi. Malengo hayo ni kama yafuatayo:

a. Kubainisha sifa za sajili ya maafisa wa polisi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.
b. Kuchunguza uamilifu wa sajili ya maafisa wa polisi, kwa maafisa wa polisi wenyewe na kwa wananchi.
**c.** Kubainisha athari zinazotokana na sajili ya maafisa wa polisi.

## 1.4 NADHARIA TETE ZA UTAFITI

a. Kwamba sajili ya maafisa wa polisi inahusishwa na matumizi ya msimbo, kuchanganya ndimi, na sauti yao hudhihirisha mamlaka.

b. Sajili ya maafisa wa polisi ina uamilifu fulani katika utekelezaji wa majukumu yao.

c. Kuwa utafiti huu utabainisha athari zinazotokana na sajili ya maafisa wa polisi kwa wananchi.

**1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA**

Makundi mbalimbali ya kijamii huwa na namna yao ya kipekee ya kuwasiliana. Maafisa wa polisi kama kikundi cha kijamii wana upekee wao wa kuwasiliana. Lugha inaweza kutumiwa kutambulisha kikundi hiki cha maafisa wa polisi.

Maafisa wa polisi wana jukumu la kulinda sheria za nchi. Chombo muhimu cha kuwawezesha maafisa wa polisi kuafikia malengo yao ni namna watakavyotumia lugha. Hii inatuelekeza katika utafiti huu-namna polisi hutumia chombo hiki muhimu katika kulinda sheria za nchi.

Kikundi hiki cha kijamii kinaweza kutofautishwa na vikundi vingine katika mkabala wa lugha yao. Kama asemavyo Gumperz (1972: 219),

> kikundi cha watu ambao wana sifa ya kuwa na mawasiliano yanayoendelea
> kila mara miongoni mwao kwa kutumia kundi lile lile la ishara za sauti,
> kikundi hicho cha watu kinatofautishwa na vikundi vingine kama hivyo kwa tofauti
> ya matumizi ya lugha. (TY)

Kutokana na maelezo haya ya Gumperz, kikundi fulani huwa na lugha yake ya kipekee kutokana na mazoea ya muda mrefu, kuishi pamoja na kushirikiana. Kwa sababu hii kikundi huwa na makubaliano yasiyo rasmi lakini ambayo yanawatambulisha. Hii inaonyesha kuwa lugha ya kikundi fulani inaweza kubainishwa na kutumiwa kukitambua kikundi hicho. Ndio maana mada hii inaweza kushughulikiwa.

Maafisa wa polisi hutumwa kufanya kazi popote nchini Kenya bila kuzingatia walikozaliwa na lugha yao ya kwanza. Kwa hivyo, katika vituo mbalimbali vya polisi huwa na maafisa wa polisi wanaotoka jamiilugha tofautitofauti na hivyo wanalazimika kutumia lugha itakayoeleweka na watu wote. Hata hivyo, wao hutumia lugha kwa njia inayotambulisha kikundi chao, hutumia lugha kwa namna tofauti na jamii wanayoitumikia. Lugha wanayoitumia yaweza kubainishwa. Maafisa wa polisi hutumia lugha ili kupata ufahamu wa jambo lililoenda kombo katika jamii kwa kuwahoji wananchi ambao pengine ni washukiwa au waathiriwa na kwa sababu hii, lugha ndicho chombo muhimu.

Ingawa sajili ya maafisa wa  polisi ni muhimu katika jamii, utafiti wa kina haujaweza kufanywa nchini Kenya kwa kuichanganua na kuibainisha sajili hiyo katika utekelezaji wa majukumu ya maafisa wa polisi. Pia yaliyoandikwa kuhusu sajili ya maafisa wa polisi nchini Kenya ni machache mno, hivyo utafiti huu utaongezea tafiti ambazo zimefanywa.

**1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI HUU**

Tulichunguza sajili ya maafisa wa polisi katika kituo cha Central mjini Nairobi wanapozungumza na wenzao na wanapowahudumia wananchi katika kituo hicho ili kubaini matumizi ya lugha yao. Tulichunguza maafisa polisi wanapozungumza hasa na raia na wanapozungumza wenyewe kwa wenyewe.

Tulichagua kituo cha polisi cha Central kwa sababu hicho ndicho kituo kikubwa nchini. Pili, kituo hiki huwa na shughuli nyingi zinazoendelea kule na hii ilituwezesha kufanya utafiti wetu.

Tatu, kituo hiki huwa na maafisa wa polisi kutoka vitengo mbalimbali kama vile trafiki, wale wa kawaida, wa utawala na hata wa upelelezi.

Tumejifunga katika kituo cha polisi cha Central kwa kuwa muktadha wake ni rasmi. Hata hivyo, matumizi ya lugha ya maafisa wa polisi hubadilika wanapokuwa nje ya kituo cha polisi. Hii inaonyesha kuwa afisa wa polisi anapokuwa nje ya kituo cha polisi huzungumza kwa njia ambayo ni tofauti.

Katika utafiti huu, tumechunguza namna kipengele cha lugha hutumiwa katika kuwatambulisha maafisa wa polisi kama kikundi maalum cha kijamii. Hatukujikita katika lugha ya maafisa wa polisi wanapokuwa nje ya kituo cha polisi ila wanapokuwa katika mazingira ya kazi ya kituo cha polisi cha Central ili kujaribu kuelewa na kuchanganua sajili ya maafisa wa polisi. Habari za kiusalama na zisizohitaji kutolewa tumezibana. Kwa hivyo, tumechanganua data inayohusu mambo ya kijumla na ambayo hayatakuwa na athari hasi baadaye.

**1.7.0 NADHARIA**

Katika utafiti huu, tumechunguza mambo kadha yanayohusiana na maafisa wa polisi. Kwa sababu hii, tulitumia nadharia zaidi ya moja. Msisitzo ulikuwa katika kutambua nadharia itakayotumiwa kuchambua sajili ya maafisa wa polisi. Tumetumia nadharia zaidi ya moja kwa kuwa mawasiliano baina ya maafisa wa polisi yanatofautiana na wanapowasiliana na raia. Tofauti imejitokeza maafisa wa polisi wanapowasiliana na wahalifu na pia wanapowasiliana na waliofika kuripoti. Kwa sababu hii, tumetumia nadharia tatu huku kila moja ikiwa na jukumu lake.

### 1.7.1 NADHARIA YA BERNSTEIN

Nadharia hii ya isimujamii inahusu misimbo. Msimbo hurejelea upangaji wa kanuni ambazo hutumiwa na watu wa kikundi fulani cha jamii wakati wa kutumia lugha ile ile kwa ajili ya mawasiliano. Kwa sababu hii, mahusiano ya watu huweza kuathiri aina ya lugha na matumizi ya lugha katika kikundi hicho.

Nadharia hii inahusishwa na Basil Bernstein (1971). Bernstein anaeleza kwamba, matumizi ya lugha ya kila siku yanaakisi na kuonyesha hali halisi ya chukulizi kuhusu utambulisho wa kikundi fulani. Kikundi husika huweza kuathiri matumizi ya lugha ya mtu binafsi ili aweze kutambulika katika kikundi hicho. Bernstein anasema kuwa lugha ni kitu cha kimsingi katika kuanzisha na kuimarisha namna ya kufikiri, hisia na tabia ambazo uhusishwa na makundi ya kijamii.

Kwa mujibu wa anayoyasema Bernstein, sura za lugha inayozungumzwa huku watu wakiwa wanafundishwa huwafanya wawe na mahusiano fulani maalum yanayohusishwa na mazingira yao. Hii inaonyesha kuwa lugha anayotumia mtu huweza kutambulisha nafasi yake katika jamii.
Bernstein anachukulia lugha kama kaida zilizoidhinishwa ambapo misimbo ya usemi hutumika. Misimbo hii ya usemi hutokana na mfumo wa mahusiano ya kijamii. Kulingana naye, muundo wa uhusiano wa kijamii huwa maalum kutokana na kinachosemwa, kinasemwa wapi na namna kinavyosemwa.

Katika mtazamo wa isimu-jamii, ni wazi kuwa watu huweza kujua majukumu yao kupitia mawasiliano ambapo majukumu hayo ni ule uelewa wa pamoja wa kikundi fulani.

Bernstein anazungumzia misimbo miwili; msimbo pana na msimbo finyu. Kiisimu, msimbo pana unahusu kuwepo kwa mawanda mapana katika uteuzi na ubashiri wa vipengele vinavyozungumziwa na kwa hivyo uwezekano wa kubashiri huwa umepunguzwa. Katika msimbo pana kila kitu husemwa waziwazi ili kila mtu aweze kuelewa ilhali msimbo finyu mawanda ni finyu na uwezekano wa watu walio nje ya kundi hilo kuelewa kinachosemwa huwa umepunguzwa.

Msimbo finyu huleta hali ya umoja. Msimbo huu huwa umebanwa na wanaolewa ni walio katika kikundi hicho husika. Huwafanya watu wanaotumia lugha kuhisi kuwa ni wa kikundi fulani. Msimbo finyu hutenga watu wasio katika kundi hilo na huwa ni njia moja ya kuhifadhi siri za kundi husika.

Nadharia ya isimujamii ya misimbo , imetuwezesha kutambua ikiwa maafisa wa polisi hutumia msimbo finyu ambao hulenga utoaji wa maana kwa kutumia maneno ambayo yanaoana na muktadha wa mazungumzo na ambayo yanaeleweka na watu wa kikundi hicho mahsusi au wanatumia msimbo pana ili kila mtu aweze kuelewa. Hii ni kutokana na maoni ya Bernstein (1971: 125) kuwa:

> kadri mtu anavyojifunza kuhusisha tabia yake na msimbo wa kiisimu, ambao ndio dhihirisho la majukumu, taratibu mbalimbali za uhusiano hujitokeza. Ni kupitia Kwa msimbo maalum wa kiisimu ndio uhusiano hujengeka, uzoefu wa muundo fulani ndio huthibiti utambulisho wa kikundi hicho. (TY)

Katika utafiti huu, hii nadharia imekuwa ya muhimu kwa sababu maafisa wa polisi huwa baadhi ya vikundi katika jamii. Kwa hivyo, wao pia hutumia lugha na misimbo inayowatambulisha kama kikundi mahsusi na misimbo huwa muhimu katika ujenzi wa uhusiano wa kijamii, namna washiriki wanavyojieleza na wanavyoithibiti. Hii imetusaidia katika kuelewa namna maafisa wa polisi hutumia misimbo yao na namna misimbo hiyo hujenga uhusiano baina ya washiriki. Imetusaidia kuelewa pia wakati na hali ambazo huwafanya maafisa wa polisi kutumia msimbo finyu au pana.

### 1.7.2 NADHARIA YA MAAFIKIANO

Nadharia ya Bernstein haitoshi kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi kwa kuwa kikundi hiki kinahusisha watu tofauti kutoka jamiilugha na matabaka tofauti ya kijamii lakini huweza kutumia lugha kwa namna moja wanapokuwa kazini. Maafisa wa polisi hufuata mtindo mmoja wa kutumia lugha, kwa sababu hii, tumeweza kuelewa sababu inayowawezesha kutumia lugha kwa namna moja kwa kutumia nadharia ya maafikiano.

Nadharia ya maafikiano iliasisiwa na Howard Giles (1987). Anasema kuwa, watu wanapoingiliana, huweza kubadili usemi wao, utumiaji wa sauti na ishara zao ili kuafikiana na wengine katika kikundi hicho. Mabadiliko haya hutokea kwa watu binafsi ambao wamejiunga na polisi ili kuweza kuafikiana na maafisa wengine wa polisi.

Nadharia hii inatalii sababu za watu binafsi kupunguza mipaka ya kijamii baina yao na washiriki wengine katika mazungumzo kupitia kwa wanayoyasema na ishara zao za kimawasiliano. Haijihusishi tu na uhusiano baina ya muktadha wa utambulisho, lakini pia, huhusishwa na

mahusiano baina ya kikundi fulani na mtu binafsi kwa kuangazia vipengele vinavyopelekea kuwepo kwa maafikiano.

Msingi wa nadharia hii ni, mtu binafsi kupunguza tofauti za usemi baina yake na kundi analohusishwa nalo. Kupunguza tofauti za matumizi ya lugha huwa njia moja ya kujitambulisha na kundi hilo husika. Maafikano hutegemea hali na kiwango cha kiisimu ambacho kinawezesha maafikiano.

Watu wanaopenda kutambulishwa na kundi fulani huweza kuafikiana na washiriki wa kundi hilo kwa urahisi kuliko wale wasiopenda kundi hilo, hasa ikiwa mtu amelazimishwa kujiunga na kundi fulani kikazi, huchukua muda kutumia lugha na kuwa na tabia zilizo sawa na washiriki wa kundi hilo. Hata hivyo, hatuna uhakika ikiwa mtu hulazimika kuwasiliana kama washiriki wa kundi lake, au hilo ni jambo ambalo huja tu kwa hiari ili kupunguza tofauti baina yao.

Giles anaendelea kusema kuwa, ili kuweza kuafikiana na watu wa kundi husika, watu huwa na uwezo wa kiisimu ambao huwawezesha kuwa kama washiriki wengine wa kundi hilo.
Nadharia hii inashughulika na vipengele viwili, navyo ni:

a. Uhusiano baina ya lugha, muktadha na utambulisho.
b. Masuala ya kikundi na ya mtu binafsi ambayo hupelekea uwepo wa maafikiano na vilevile namna miktadha ya kimakro na kimaikro inavyoathiri tabia za kiusemi.

Mambo haya ni muhimu katika kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi kwa kuwa yametusaidia kuelewa maafikiano baina ya maafisa wa polisi hasa wanapokuwa katika mazingira yao ya kazi, katika kituo cha polisi.

Giles anaelezea dhana mbili:

a. Mwingiano: ambapo anasema kuwa ni hali ambapo watu huendelea kuafikana kwa namna ya kuzungumza na ishara ili kupunguza tofauti baina yao. Kwamba mtu huacha vile alivyozoea kuzungumza na kufuata mtindo wa washiriki wengine katika kikundi hicho.
b. Ulahajishaji: hii ni hali ya kuongezeka kwa tofauti katika lugha hadi kufikia hatua ya kutokea lahaja, (TUKI 1990: 21). Kulingana na Giles, ulahajishaji ni hali ambapo mtu binafsi hutilia mkazo tofauti za kiusemi na kiishara baina yake na washiriki wengine wa kundi hilo. Hii inaonyesha kuwa hataki kuzungumza au kuwasiliana kama wanaovyowasiliana washiriki wengine wa kikundi hicho. Kwa kufanya hivi, mtu huyo hawezi kutambulishwa na kundi hilo kwa kuwa hamna maafikiano baina yake na wenzake.

Katika utafiti wetu, tumejikita katika dhana ya mwingiano kwa sababu, kadri mtu binafsi anavyojihusisha na mwingiano katika kundi fulani ndivyo maafikiano baina yake na washiriki wengine huongezeka na hii huashiria kuwa amekubali kazi anayoifanya na kukubali kuwa katika kikundi hicho. Inaaminika kuwa maafisa wa polisi kama kikundi cha kijamii huwa na mtindo mmoja wa kuzungumza. Kwa hivyo, yule anayejiunga nao hana budi kuafikiana na washiriki wengine kama njia ya kujitambulisha na maafisa wa polisi.

Ulahajishaji pia umekuwa muhimu kwetu hasa tunapobainisha mazungumzo baina ya maafisa wa polisi na wateja wao. Wateja hutumia lugha kwa namna walivyozoea na ndio maana utampata akizungumza kwa lugha sanifu kinyume na ilivyo afisa wa polisi anayemshughulikia ambaye anaweza kuchanganya ndimi.

Nadharia hii pia ni muhimu katika utafiti wa sajili ya maafisa wa polisi nchini Kenya, kwa sababu maafisa wa polisi kama kikundi cha kiisimu wanaweza kutambuliwa kutokana na namna wanavyotumia lugha. Kikundi ambacho kinaweza kutambuliwa kiisimu huwa na njia zao za kipekee za usemi ambazo huwatofautisha na makundi mengine. Nadharia hii imesaidia katika kuelewa ikiwa pana maafikiano baina ya maafisa wa polisi kwa kujikita katika njia zao za kutumia lugha.

Kama anavyosema Giles, maafikiano yanaweza kuwa yakitumiwa na wazungumzaji ili kuweza kuelewana. Kuelewana huku husaidia katika utekelezaji wa majukumu bila mushkili wowote kwa kuwa washiriki hawa huwa na umoja. Umoja huu huweza kujitokeza katika matumizi yao ya lugha. Nadharia hii imekuwa muhimu kwetu kwani imetuwezesha kuelewa kama pana maafikiano baina ya maafisa wa polisi.

### 1.7.3 NADHARIA YA VITENDO USEMI

Nadharia za Bernstein na Giles hazitoshi katika kuchanganua lugha ya maafisa wa polisi kwa kuwa wanapotoa usemi, hutaka kitendo fulani kitendwe. Kwa mfano, wanapowashika wahalifu, huwaambia 'Keti chini, au inua mikono.' Wahalifu hawa hutenda wanachoambiwa pasi na

kuzungumza, ndiposa nadharia hii ya vitendo usemi imekuwa muhimu kwani imetuelekeza katika kuchunguza umuhimu wa mawasiliano kwa njia ya vitendo. Kama asemavyo Schiffrin (1994: 59):

> Mawasiliano hutegemea mambo yanayojulikana kuhusiana na jina na vitendo usemi; Mzungumzaji na mzungumziwa huwa na uzoefu sawa wa namna ya kutambua na kubainisha usemi kama kitendo fulani, kama kipengele cha lugha kinachotolewa na hufasiriwa kulingana na kanuni za vijenzi.(TY)

Schiffrin anasema kuwa kuwasiliana kwa kutumia vitendo, hutegemea uelewa wa makundi yote mawili. Anayeambiwa atende jambo fulani, hulitenda kwa kuwa anaelewa alichoambiwa afanye. Maafisa wa polisi huwaambia raia kutenda vitendo wanavyovijua au walivyozoea. Kwa kufanya hivi, huwa wanadhihirisha mamlaka fulani.

Nadharia hii inasema kuwa lugha hutumiwa katika kutenda vitendo. Hii ina maana kwamba katika matumizi ya lugha kuna vitendo fulani vinavyotendwa. Vitendo hivi hutendeka katika muktadha, hali na mazingira mahsusi.

Nadharia hii imeasisiwa na wanafilosofia wawili; Austin na Searle.Wanaona mazungumzo katika lugha kama kauli ambazo ukweli au uwongo wake hutokea kwa njia ya vitendo. Nadharia hii huwa na vitendo usemi. Searle (1975) anasema kuwa kitu cha kimsingi katika mawasiliano ni vitendo usemi, ambavyo huwa mzizi wa kuchunguza maana ya usemi katika mawasiliano. Katika utafiti huu, nadharia ya vitendo usemi imetuwezesha kutambua hali

zinazokumba utoaji wa usemi kama kitendo cha kiisimu. Kwa hivyo nadharia hii imekuwa muhimu katika kuchambua usemi wa maafisa wa polisi.

Nadharia hii imetusaidia katika kuchanganua sajili ya maafisa wa polisi, namna wanavyotumia kanuni na hali zinazofumbatwa katika vitendo mahsusi. Tumechunguza mambo yanayosababisha kutokea kwa vitendo baada ya usemi fulani. Pia imetuwezesha kuelewa sababu ya maafisa wa polisi kuamua kutumia usemi utakaopelekea utendaji wa vitendo.

Utendaji huu wa vitendo unaonyesha namna maana na vitendo uhusiana katika lugha. Kulingana na Austin, kila hatua ya lugha inatenda kitendo fulani. Anaendelea kusema kuwa katika matumizi sawasawa ya lugha, vitendo hivi huwa kadha;

a. Vitendo vya Lokusheni: vitendo hivi anavifafanua kuwa ni utoaji wa sauti na maneno yenye maana, kuanzia safu ya fonolojia hadi maana. Kwamba ni matumizi sahihi ya lugha
b. Vitendo vya Ilokusheni: hivi ni vitendo vinavyotendwa baada ya kusema lokusheni.
c. Vitendo vya Palokusheni: hii ni athari ya usemi kwa washiriki.

Katika vipengele hivi, ni kuwa kwa kutoa usemi, ni lokusheni, kwa kutenda ulichokisema ni ilokusheni na katika palokusheni, ni athari kwa washiriki.

Kwa upande mwingine, Searle (1975), anasema kuwa kipengele cha kimsingi katika mawasiliano ni vitendo usemi ambavyo anaviona kuwa ni kiini cha utafiti wa maana ya lugha na mawasiliano.

Katika utafiti huu, nadharia ya vitendo usemi, imesaidia katika kuelewa masharti ya kutoa usemi na kuelewa usemi kama kitendo cha kiisimu. Hii imetusaidia katika kuchunguza usemi unaotumiwa na maafisa wa polisi, kuangalia namna vitendo hivyo vinavyohusiana na kanuni na masharti ya vitendo fulani; kuchunguza namna usemi unavyopelekea kutokea kwa vitendo na hivyo kujaribu kuelewa kwa nini hutumiwa na maafisa wa polisi.

## 1.8YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Vahid na wengine (2008) wanaonyesha usemi wa maafisa wa polisi wa trafiki. Walichunguza umuhimu wa cheo na usemi kwa kujikita katika uteuzi wa maneno na kiimbo cha mzungumzaji. Walipata kuwa, namna watu hutumia lugha na kuieleza husababishwa na tishio, kushurutishwa na pia ili kuweza kuwapunja wengine. Walichunguza usemi wa polisi wa trafiki na madereva ili kuchanganua ubaguzi au dhuluma za matumizi ya lugha kiisimu baina ya wahusika. Waliwahoji madereva waliotozwa faini na ambao waliweza kufichua vitendo visivyo halali vinavyotendwa na maafisa wa polisi wa trafiki. Walipata kuwa, maafisa wa polisi wa trafiki, walitumia lugha ili kuonyesha mamlaka yao na hatimaye waliweza kupewa hongo. Pia walipata kuwa, walitumia lugha kuwaeleza madereva hatima ya vitendo vyao hasa waliokataa kuwahonga.

Utafiti wao unatofautiana na wetu kwa kuwa sisi tumewachunguza maafisa wa polisi wa vitengo mbalimbali wanaopatikana katika kituo cha polisi cha Central, pili, sisi tumetumia mbinu ya kurekodi kinyume na wao walivyotumia mahojiano. Hata hivyo, utafiti wao umechangia katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu umetuwezesha kuchunguza namna maafisa wa polisi hutumia lugha yao ili kutekeleza majukumu yao na kudhihirisha mamlaka yao.

Leach na Silva (2006), Walichunguza kiwango ambacho maafisa wa polisi na watu wa kawaida wanavyoweza kugundua udanganyifu katika usemi kwa wazungumzaji wa Lugha ya pili. Watafiti hawa walijikita katika udanganyifu au ukweli wa jambo fulani aidha katika lugha ya kwanza au lugha ya pili. Walipata kuwa polisi hugundua udanganyifu katika watumizi wa lugha ya kwanza kwa urahisi kuliko kwa watumizi wa lugha ya pili. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa tumechunguza lugha ya maafisa wa polisi na wala si kuchunguza namna wanavyogundua udanganyifu kwa kutegemea lugha inayotumiwa na wazungumzaji, ila utafiti huu umetufaa si haba.

Michira (1993) alishughulikia usemi wa Kiswahili. Katika utafiti wake aliangalia kuchanganya ndimi katika matumizi ya lugha ya Kiswahili sahihi ya wachuuzi katika soko la Gekomba na matangazo ya biashara yanayotangazwa kwa Kiswahili katika redio. Katika utafiti wake, alipata kuwa wachuuzi na matangazo ya biashara redioni husheheni kuchanganya ndimi. Utafiti huu umetufaa ila unatofautiana na wetu ambao unahusu sajili ya maafisa wa polisi. Hii ni kutokana na kuwa sajili ya maafisa wa polisi husheheni matumizi ya kuchanganya ndimi.

Habwe (1999) alichunguza lugha katika siasa. Anasema kuwa hotuba za kisiasa zinakuwa changamano kwa kuwa hadhira na mzungumzaji wanahusika pakubwa katika kuendeleza hotuba. Anaendelea kusema kwamba, hadhira huweza kuathiri mwelekeo wa mada ya hotuba. Anasema kuwa, hatibu katika mkutano wa kisiasa sharti aweze kutilia maanani matakwa ya hadhira la sivyo wanaweza kuondoka mkutanoni. Kwa sababu hii, wanasiasa hutumia lugha shawishi ili kuteka fikra za hadhira yao.

Utafiti wetu unatofautiana na wa Habwe kwa kuwa sisi tumechunguza lugha ya maafisa wa polisi ambao hawatumii lugha shawishi bali hupaswa kutumia amri kutokana na uhalisi wa kazi yao.

Utafiti wake umetufaa katika kuelewa lugha ya kikundi tofauti na wanasiasa, yaani maafisa wa polisi.

Mang'eli (2008) alichunguza maana ya dhana za 'Majimbo' na 'Mabadiliko' kama zilivyotumiwa katika uchaguzi wa kitaifa wa mwaka 2007 nchini Kenya kwa kutumia nadharia ya Uhusiano. Alichunguza namna dhana hizi ziliweza kutumiwa na vyama vya ODM na PNU vilivyokuwa vikiwania viti mbalimbali. Alichunguza namna dhana hizi ziliweza kuwasilishwa kwa wapiga kura na athari iliyotokana na dhana hizi. Katika utafiti wake, alipata kuwa, wapiga kura waliweza kuathiriwa ili kukubali au kukataa dhana hizi. Pili alipata kuwa, wapiga kura walifasiri dhana hizi kwa namna tofauti na tatu, wapiga kura walielewa dhana hizi kama zilivyowasilishwa kwao na chama wanachokienzi. Wafuasi wa ODM waliunga dhana hizi mkono ilhali wale wa PNU walipinga dhana hizi.

Utafiti wetu unatofautiana na wake kwa kuwa tumejikita katika lugha ya maafisa wa polisi kwa kutumia nadharia za vitendo usemi, maafikiano na nadharia ya Bernstein. Hata hivyo, utafiti huu umekuwa wa manufaa kwetu hasa kwa kuwa tunachunguza athari za lugha ya maafisa wa polisi kwa wananchi na wao wenyewe.

Njenga (2008) alitaka kuchunguza ikiwa mtazamo wa Myers Scotton, (1993) waweza kutumika katika kuchunguza ikiwa uhusiano wa kijamii huweza kuchochea kubadili msimbo kutoka kwa lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Alijikita katika mazungumzo ya redio ya Easy FM. vipindi vya 'Easy Breakfast' 'Easy Connection'na Easy Jam'. Hivi ni vipindi ambavyo watu hutoa mchango wao. Matokeo yake yanaonyesha kuwa baadhi ya kanuni za mtazamo huu wa Myers ziliweza kujitokeza katika data yake na kwa hivyo kuna ubia unaojitokeza.

Utafiti huu ni muhimu kwetu kwa kuwa kuna chukulizi kuwa sajili ya maafisa wa polisi husheheni kuchanganya ndimi na kubadili msimbo. Hata hivyo, utafiti wake unatofautiana na wetu kwa kuwa tunatumia nadharia tofauti.

Fairclough (1989) anazungumzia kuhusu umaanisho baina ya lugha na asasi za kijamii katika masuala ya kisiasa na miundo ya kijamii. Anazuka na athari za kiisimu ambazo hutokana na wasikilizaji wanaposikiza matangazo, biashara, siasa na usemi katika vyombo vya habari. Kwa kuzungumzia lugha, anasema kuwa ni matokeo ya uhusiano wa mamlaka na kupigania mamlaka. Anaona mambo haya kama uhalisi wa kawaida ambao huchukulia kuwa mamlaka na mfumo wa ngazi kama vitu halisi. Anatoa mfano wa chukulizi hizi ambao ni itikadi. Anasema kuwa itikadi uhusishwa na mamlaka, kwa sababu, uhalisi wa chukulizi za itikadi hufungamanishwa na mapatano kutegemea na uhusiano wa mamlaka ambao huleta mapatano hayo. Anasema kuwa itikadi fulani huhalalisha uhusiano uliopo wa kijamii na tofauti za mamlaka. Kulingana naye, hii husababishwa na mazoea na tabia zinazofanana ambazo huwafanya watu kuchukulia mahusiano haya kimzaha. Fairclough anaendelea kusema kuwa itikadi huhusishwa na lugha.

Maoni ya Fairclough ni muhimu katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu, maafisa wa polisi hutumia lugha kwa namna moja kutokana na uhusiano wao na pia kutokana na uhalisi wa kazi yao ambayo huwapa mamlaka. Maoni haya yametusaidia katika kuchunguza lugha ya maafisa wa polisi ambayo inawatambulisha wao kama kikundi cha kiisimu.

Tumechunguza kama mamlaka walio nayo maafisa wa polisi huwafanya kuzungumza kwa namna fulani. Mamlaka haya huathiri jamii husika, kwa kuwa maafisa wa polisi hutumia lugha kwa namna ya kipekee kwa kuwa wana mamlaka fulani ambayo Fairclough anayaita maafikiano 'asilia.'

Maoni ya Fairclough yametusaidia katika kutambua sajili ya maafisa wa polisi kwa kujikita katika muktadha wao wa kazi. Anasema kuwa itikadi hujitokeza katika lugha na ndio maana itikadi asilia za lugha zapaswa kuwa maudhui muhimu katika sayansi ya kijamii.

**1.9 MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ni wa nyanjani. Ilitubidi kuenda kwenye kituo cha polisi cha Central katika jiji kuu la Nairobi ili kuweza kuchunguza lugha wanayoitumia maafisa wa polisi katika utendakazi wao. Tulienda kwa wanaorekodi matukio, wale wanaohusika na washukiwa kwenye seli na mahali ambapo maafisa hawa walikuwa wakizungumza wenyewe. Tunachunguza sajili ya maafisa wa polisi wa kawaida,wale wa upelelezi, wa trafiki na wale wa utawala.

### 1.9.1WALENGWA

Hiki ni kikundi kizima cha kutafitiwa.Maafisa wa polisi wanaofanya kazi katika kituo cha Central ni 335. Hawa ndio walengwa wetu, ila hatukuweza kuwarekodi wote bali tumetumia sampuli kielelezo.

### 1.9.2 SAMPULI KIELELEZO

Idadi ya maafisa wa polisi wanaofanya kazi katika kituo cha Central ni 335. Ni vigumu kuweza kuwapata wote kwa ajili ya utafiti huu. Kwa hivyo, tulitumia kikundi kidogo kutoka kwa kikundi hicho kizima ili kutuwezesha kuafikia lengo letu. Kulingana na Mugenda Mugenda (2003) anasema hiki kikundi kidogo ni sharti kiwe asilimia 30 ya kikundi kizima. Kituo cha polisi cha Central kina jumla ya polisi 335, kupata kikundi kidogo katika utafiti ilikuwa maafisa 100 kama inavyojitokeza katika jedwali 1

**Jedwali 1.1**

| Idara | Walengwa | Sampuli |
|---|---|---|
| Polisi wa kawaida | 205 | 61 |
| Polisi wa upelelezi | 70 | 21 |
| Polisi wa trafiki | 30 | 9 |
| Polisi wa utawala | 30 | 9 |
| Jumla | 335 | 100 |

Katika utafiti wetu, tulitumia maafisa wa polisi 100 kutoka idara mbalimbali za polisi zinazopatikana katika kituo cha Central. Kwa siku tulirekodi maafisa wa polisi 8. Tulikwenda

kwenye kituo hiki mara 13. Baada ya kuzuru kituo cha polisi cha Central, tulieleza na kuchanganua data tuliyoipata.

Tulitumia maafisa wa polisi 100 kwa kuwa muda tuliotumia kuwarekodi ulitegemea muda waliotumia kuzungumza. Hatukuweza kutumia muda zaidi ya ule wa mazungumzo yao kwa kuwa wakishafumukana nasi tuliondoka.

### 1.9.3MBINU ZA UKUSANYAJI DATA

Utafiti huu ni wa nyanjani na hivyo, tulienda katika kituo cha Central wanakofanyia kazi yao kisha tulirekodi waliyoyasema bila wao kugundua ila mmoja wao ambaye alikuwa akituongoza. Nilikwenda pale kama mteja wao kisha nilirekodi mazungumzo yetu. Baadaye, tulichanganua data hiyo. Maswali fulani yalituwezesha kufikia lengo letu:

a. Je, sajili ya maafisa wa polisi wanapokuwa katika kituo cha polisi ni ipi?

b.Je, sajili ya maafisa wa polisi ina uamilifu wowote katika jamii?

c. Ni athari zipi hutokana na sajili ya maafisa wa polisi kwa jamii?

Baadaye tulitumia hiyo data kuichambua na kuibainisha sajili ya maafisa wa polisi kwa mujibu wa nadharia tunazotumia.

Katika sura hii, tumeonyesha mambo muhimu kuhusu utafiti. Tumeonyesha nadharia tunazozitumia katika utafiti wetu na pia kuonyesha umuhimu wake. Pia tumeonyesha mbinu tulizozitumia katika utafiti wetu. Tunasonga mbele na kuanza kuchanganua sajili ya maafisa wa polisi kwa mujibu wa nadharia tulizofafanua katika sura hii.

# SURA YA PILI

# DHANA MUHIMU ZA SAJILI YA MAAFISA WA POLISI

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumeangazia dhana muhimu katika utafiti wetu. Dhana hizi ni za isimujamii na kwa hivyo, tumeanza kwa kufafanua dhana ya isimujamii. Pia, tumefafanua dhana za jamii, na sajili na kutoa baadhi ya mifano ya sajili zinazoangaziwa na wanaisimu mbalimbali. Mifano hii ya sajili itatuwezesha kujenga msingi katika utafiti wetu. Tumeangazia dhana hizi kwa kujikita katika maoni ya wanaisimu mbalimbali. Katika utafiti wetu tunachunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili na kwa hivyo, hatuna budi kuingazia lugha hii na pia kuonyesha sababu ya kuamua kuitumia katika utafiti wetu.

## 2.1 DHANA YA ISIMUJAMII

Isimujamii ni neno lililoundwa kwa maneno mwambatano; isimu na jamii. Isimu ni taaluma ya uchanganuzi wa kisayansi wa lugha, na jamii ni kundi la watu ambao wameunganishwa na tamaduni, kaida na matumizi yao ya lugha. kundi hili la watu huwa na sifa ambazo zinaweza kutumiwa kulitambulisha. Isimujamii nayo ni taaluma ambayo Mekacha (2011: 23) anasema kuwa inajishughulisha na kutafiti, kuchanganua na kufafanua uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii. Kulinganana Mekacha, isimujamii hujishughulisha na utafiti wa lugha katika jamii fulani kisha kuichanganua na kuifafanua ili kuiweka wazi. Maoni yake ni muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa tunatafiti kuhusu sajili ya maafisa wa polisi kwa kujikita katika matumizi yao ya lugha ya Kiswahili.

Hudson (1980:1) anasema kuwa isimujamii ni taaluma inayochunguza lugha kwa kujikita katika jamii. Nao Iribemwangi na Mukhwana (2011: 19) wanasema kuwa “isimujamii hujihusisha na masuala ya kilugha yaliyo katika hali halisi katika muktadha mahsusi wa kijamii.” Wataalamu hawa wanaonyesha kuwa isimujamii ni taaluma inayochunguza lugha inayotumiwa na jamii fulani katika muktadha fulani mahsusi. Muktadha au mazingira ambamo mazungumzo hufanyika huwa na athari kubwa kwa aina ya lugha itakayotumika. Mkondo wa mazungumzo wa watu hutofautiana kutegemea na mahali walipo. Kwa mfano, katika matanga, mazungumzo ambayo hutawala huwa ni ya kuliwaza waliofiwa na kusifu marehemu ilhali katika mikutano ya kuhubiri amani, mazungumzo huhusu namna ya kukomesha uhasama, kuwasuta wachochezi na pia kueleza umuhimu wa kuishi pamoja kwa amani. Mifano hii inaonyesha kwamba muktadha wa mazungumzo humwezesha mzungumzaji kuteua mada mwafaka na pia kutumia lugha kwa njia inayoafiki muktadha husika. Katika matanga, mzungumzaji huwasilisha ujumbe wake kwa kutumia sauti ya kuliwaza ila katika mikutano ya kuleta amani, wazungumzaji wanaweza kutumia ukali hasa wanapowasuta wachochezi na kuwaonya kwamba watachukuliwa hatua za kinidhamu. Hii ndio sababu tuliamua kufanya utafiti katika kituo cha polisi kwa kuwa haya ndio mazingira ya kazi.

Maafisa wa polisi wanapozungumza wenyewe huwasiliana kwa namna tofauti na wanapozungumza na washukiwa. Wanapozungumza wenyewe hujadili masuala yanayowahusu. Wanapozungumza na waliofika kuripoti jambo pia huzungumza wakiwa rasmi ila wanapozungumza na washukiwa hata sauti zao hubadilika kwa kuwa wanawataka washukiwa kutii amri.

Kuna uhusiano baina ya lugha na jamii. Mfumo wa kijamii waweza kuathiri au kubainisha mfumo wa kiisimu na tabia za kundi fulani la kijamii. Lugha ambayo jamii hutumia huashiria kikundi chao. Hii ni kwa sababu, watu katika kikundi huwasiliana kwa namna fulani kutokana na majukumu yao katika jamii. Maafisa wa polisi huwasiliana kwa namna ya kipekee na ndio maana wanaweza kutambuliwa kama kikundi cha kijamii. Kikundi hiki cha kijamii kinaweza kutambuliwa kutokana na lugha wanayoitumia katika mazingira mahsusi ya kazi. Katika utafiti wetu tunaangazia kikundi cha maafisa wa polisi kwa kujikita katika mazungumzo yao; wanazungumza na nani, wapi na vipi. Hii ni kutokana na kuwa kuna namna tofauti ya kuwasiliana na kueleza kitu kile kile katika makundi mbalimbali ya kijamii.

Tunatumia mwelekeo wa isimujamii kwa kuwa ni taaluma inayohusika na uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii. Hudson (1980: 13) anasema kuwa kuna ithibati tosha kuwa muundo wa jamii umetokana na isimujamii, kama vile, jamii hugawanywa na kutambuliwa kwa kutumia umri, chimbuko, cheo, jinsia, au kazi wanazozitenda. Katika utafiti wetu tumejikita katika kazi wanayoitenda maafisa wa polisi yaani kazi ya kulinda usalama wa nchi na pia kukomesha ghasia.

Wanapofanya kazi, maafisa wa polisi hulazimika kutumia lugha kwa namna tofauti kutegemea na wanazungumza na nani na wapi. Kutokana na uhalisi wa kazi yao, maafisa wa polisi huingiliana na watu wa matabaka yote na wanaofanya kila aina ya kazi nchini. Hutangamana na maafisa wa ngazi za juu serikalini, walevi, wafanyabiashara wakubwa na wadogo na raia wengine na hata wasiokuwa na kazi kama vile vijana wa mtaani. Watu hawa wote hutaka

kuhudumiwa na pia kusikizwa na maafisa wa polisi. Jambo muhimu ni namna maafisa wa polisi watakavyowasiliana nao kutegemea ni nani na amefika kituoni kwa nini.

Katika mtazamo wa kiisimujamii, Iribemwangi na Mukhwana (2011: 13) wanasema kuwa "lugha huchukuliwa kama sehemu ya utamaduni wa jamii. Utamaduni huo una utaratibu mahsusi na hurithishwa na watu wenyewe kutoka kizazi kimoja hadi kingine." Maafisa wa polisi ni kikundi cha kijamii. Katika kuangalia sajili yao, tunagundua kuwa lugha inaweza kutumiwa kuwatambulisha. Hii ni kutokana na namna ya kipekee wanayotumia kuwasiliana. Namna hii ya kipekee ya kuwasiliana, ndio nguzo ya utafiti wetu.

Maafisa wa polisi hutoka katika jamiilugha tofautitofauti, matabaka mbalimbali na walio na viwango tofauti vya elimu. Hata hivyo, wanazungumza kwa namna moja kutokana na kuwa pamoja, kufanya kazi sawa, wana malengo sawa na pia wana tajriba sawa. Kwa mujibu wa Hudson (1980: 177) ni kuwa mtu binafsi anaweza kutumia lugha kama washiriki wenzake katika kikundi kutegemea na kiasi alichoathiriwa na mazoea ya kuwa pamoja. Mazoea huwafanya kuwa jamii moja ambayo inaweza kutambuliwa. Maafisa wa polisi hufanya kazi pamoja, kwa sababu hii, wanaathiriana wakiwa wanajua au pengine bila wao kugundua.

Kama asemavyo Fishman lengo la isimujamii ni kufafanua nani anatumia lugha gani na nani, wakati gani na kwa namna gani. Maoni haya yanaonyesha kuwa mchakato wa mazungumzo huchochewa na mazingira, washiriki wa mazungumzo hayo. Lengo la mazungumzo hayo huathiri namna mawasiliano yatakavyoendeshwa. Kwa sababu hii, utafiti wetu unafuata mwelekeo wa isimujamii ili kueleza sajili ya maafisa wa polisi.

## 2.2 DHANA YA JAMII

Katika utafiti wetu, tunatumia neno jamii kwa maana ya kikundi cha watu ambao wameungana pamoja kwa nia ya kufanya kazi pamoja na kulinda sheria za nchi. Mekacha (2011: 18) anasema kuwa "jamii imeundwa na jumla ya mtu mmoja, kila mmoja katika upekee wake na ndiyo chimbuko la kila kitu ikiwa ni pamoja na mabadiliko katika jamii na uhusiano kati ya lugha na jamii." Jamii ni watu, kila mmoja akiwa na upekee wake ila wanapoungana na kuwa pamoja kwa sababu fulani, basi wanakuwa na tabia fulani zilizo sawa katika kutekeleza majukumu yao. Hii ni kwa kuwa wanataka kupunguza mipaka baina yao hasa katika utenda kazi wao.

Linda na Wareing (1999: 143) wanasema kuwa utambulisho wa kijamii si jambo ambalo mtu binafsi anaweza kujiamulia mwenyewe; inategemea na namna watu wengine wanavyowachukulia. Hii ina maana kwamba ni vigumu kwa mtu binafsi kujitambua mwenyewe katika kikundi fulani. Watu wengine walio nje ya kikundi hicho cha kijamii ndio hukutambulisha na kikundi hicho kutokana na kuwa na tabia fulani zilizo sawa na washiriki wengine wa kundi hilo. Wanaendelea kusema kuwa mtu binafsi anaweza tu kutambua hadhi yake katika kikundi kutegemea na cheo alichonacho. Katika kazi mbalimbali, kuna watu walio na vyeo zaidi ya wenzao. Kwa mfano shuleni, kuna mwalimu mkuu, naibu mwalimu mkuu na walimu wengine. Mwalimu mkuu ndiye kiongozi na amesimamia walimu na wanafunzi. Kazi ya polisi, inakuwa pia na maafisa wa polisi walio katika vyeo mbalimbali ikiwemo mkubwa wa kituo cha polisi, inspekta, koprol na wengineo. Hawa ndio hujitambua kwa cheo chao. Panapotokea jambo la kutangazwa katika vyombo vya habari, ni jukumu la wakubwa kufanya hivyo huku wakitajwa majina yao. Washiriki wengine, yaani maafisa wa polisi wasio na vyeo, wanapozungumza katika vyombo vya habari majina na sura zao hubanwa katika televisheni kwa madai kuwa

hawaruhusiwi kuzungumza. Hii inaonyesha kuwa utajitambua tu na kikundi hicho kutokana na cheo chako lakini kama huna cheo, basi wewe ni kama washiriki wengine wa kikundi hicho ambao hutambuliwa kuwa katika kikundi fulani na watu wengine.

Kuna mambo mengi ambayo hutambulisha watu wa kikundi fulani cha kijamii; wanaisimu hawa wametaja baadhi yao kama vile mavazi lakini pia baadhi ya mambo fulani ya kiisimu huweza kutumiwa kutambulisha kikundi cha kijamii. Maafisa wa polisi wana tabia zinazowatambulisha kama jamii moja. Hii inatokana na mazoea waliyonayo ya kazi. Fishman (1968: 170) akimnukuu Homans, anasema kadri watu wanavyoingiliana, ndivyo wanazidi kufanana katika hali fulani katika shughuli zao na mazungumzo yao huwiana. Maafisa wa polisi huingiliana wanapokuwa katika mazingira ya kazi. Mazoea haya yamewafanya kuwasiliana kwa njia ambayo inaweza kutumiwa kuwatambulisha wao kama jamii. Hii imewafanya maafisa wa polisi binafsi kupunguza mipaka baina yao na kujipata wakizungumza kwa namna moja.

Kwa hivyo, jamii ni kikundi cha watu walio na sifa fulani mahsusi ambazo zinaweza kutumiwa kuwatambulisha. Upekee wao wa kutenda au kuzungumza ni baadhi ya mambo ambayo huwafanya kuitwa jamii moja.

## 2.3 DHANA YA SAJILI

Katika utafiti huu tunajikita katika sajili ya maafisa wa polisi. Neno sajili limeweza kufafanuliwa na wataalamu wengi. Kwa mujibu wa Iribemwangi na Mukhwana (2011: 19) “sajili katika taaluma ya isimujamii humaanisha mikondo ya kimawasiliano itumiwayo katika hali na

miktadha fulanifulani kwa madhumuni fulani maalum." Wanaendelea kutaja mambo yanayoathiri sajili anayozungumzia Halliday.

a. Utaratibu wa mahusiano ya maisha. Wanasema kuwa huu ni uhusiano baina ya mzungumzaji na mzungumziwa.
b. Uwanja unaozungumziwa. Mada zinazozungumziwa na mahali zinakozungumziwa ni muhimu katika kufafanua sajili husika.
c. Mtindo au namna. Wanasema kuwa hii ni jinsi ya kufanya jambo. Katika sajili, mtindo ni njia ya mawasiliano kwa mfano, lugha iliyoandikwa au ya mazungumzo.

Wanaisimu hawa wanasema kuwa sajili hujitokeza wazi katika mazingira fulani mahsusi. Hii ina maana kuwa sajili hutofautiana kutegemea matumizi ya lugha ya kikundi fulani cha kijamii. Mtu binafsi anaweza kuwa na sajili mbalimbali kutegemea na hali yake, kazi, malengo na hata cheo chake. Mtu yuyo huyo anapokwenda matangani atatumia sajili tofauti na anapokwenda arusini. Anapozungumza na wenzake waliofika kumtembelea nyumbani atazungumza kwa namna tofauti na anapowarudi wanawe waliokosa. Sajili hizi zinatofautiana kwa kutegemea mada, muktadha, uhusiano na pia lengo la mzungumzaji. Maafisa wa polisi wana madhumuni sawa na hivyo, wanapokuwa katika kituo cha polisi wanatumia lugha kwa njia sawa.

Tukiangazia mambo waliyoyataja yaliyozuliwa na Halliday, pana tofauti kubwa wakati maafisa wa polisi wanapozungumza wenyewe na wakati wanapozungumza na wateja wao. Mada wanazozungumzia wanapokuwa wenyewe ni tofauti na wanapozungumza na mhalifu, aliyekuja kupiga ripoti na hata mshukiwa aliyefikishwa katika kituo cha polisi.

Hudson (1980: 48) anasema kuwa sajili ni matumizi ya lugha kutegemea na muktadha. Hii inaonyesha kuwa, muktadha wa mazungumzo huathiri lugha inayotumiwa. Maoni haya yanaoana na ya Trudgill (2000: 81) ambaye anasema kuwa lugha hutofautiana kutegemea tabia za wazungumzaji kama vile; tabaka, jamiilugha, jinsia lakini pia kutegemea na muktadha ambapo wazungumzaji wanajipata. Mzungumzaji yule yule anatumia lugha kwa namna mbalimbali katika hali tofauti na kwa madhumuni fulani. Maafisa wa polisi wanapokuwa katika muktadha rasmi ambao ni kituo cha polisi hutumia lugha kwa namna moja kwa kuwa hapa wana madhumuni sawa.

Trudgill (2000: 81) anasema kuwa sajili huwa na sifa za tofauti za kimsamiati kama vile, matumizi ya maneno fulanifulani au kutumia maneno kwa maana fulani. Anaendelea kusema kuwa sajili ni mfano wa aina ya lugha inayotumiwa katika muktadha fulani. Kwa sababu hii, anasema jamii huzungumza lugha kwa njia fulani kutokana na mazoea. Maoni haya ya mwanaisimu huyu yanaonyesha kuwa lugha hutumiwa kwa namna fulani kutegemea na muktadha wa mazungumzo. Muktadha wa mazungumzo ni mojawapo wa viamuzi vya lugha. Huwawezesha watu kuteua misamiati watakayoitumia ili pawepo na maafikiano baina ya msamiati na muktadha.

Kwa mujibu wa Hudson (1980: 49), kitendo cha mawasiliano hujikita katika muktadha wa wazungumzaji. Hii inaonyesha kuwa, muktadha huwezesha mawasiliano kuendelea kwa kufuata mkondo fulani wa mazungumzo. Muktadha waweza kuwa wa kanisani, kazini, shuleni au hata gerezani. Mazungumzo na uteuzi wa misamiati katika miktadha hii yatatofautiana.

Sajili inaelekea kuwa muhimu hasa katika uteuzi wa msamiati husika ili kuweza kuwiana na muktadha husika. Halliday (1978:33), alibainisha aina tatu za kanuni ambazo hutawala mazungumzo:

a. Taaluma: ambayo anasema kuwa hujishughulisha na madhumuni na mada ya mawasiliano.
b. Mtindo: hurejelea njia ya kutoa mawasiliano kwa mfano, kama ni mazungumzo au maandishi.
c. Utaratibu: hii inategemea uhusiano wa wazungumzaji.

Katika kanuni ya kwanza, mada ya mazungumzo huweza kusaidia katika kuteua msamiati ambao unakubalika katika taaluma husika. kuna taaluma zingine ambazo huhitaji mambo kusemwa waziwazi bila kutumia tasfida, taaluma zingine humhitaji mzungumzaji kutumia tasfida ili asije akawakera wasikilizaji. Stockwell (2002: 7), anasema kuwa sajili mbalimbali sharti zifungamanishwe na matarajio ya tamaduni. Tamaduni zinamhitaji mtu kutumia lugha ya heshima hasa mbele ya hadhira. Hii ndio maana tunasema kuwa muktadha ni kiamuzi muhimu katika kutambua sajili. Hivyo kanuni ya kwanza inajibu swali la kwa nini.

Kanuni ya pili ambayo ni mtindo, inaonyesha kuwa kuna tofauti wakati ambapo mtu anazungumza na wakati anapoandika. Mtu anapozungumza na washiriki wenzake katika kikundi atatateua msamiati unaoingiliana na mazungumzo yao na pia atakuwa akiafikiana na washiriki wenzake katika mazungumzo. Mtu huyo huyo anapoandika, hamna athari kutoka kwa washiriki wenzake kwa hivyo atatumia lugha kama mtu binafsi.

Kanuni ya tatu, utaratibu, inaonyesha kuwa uhusiano wa wazungumzaji hutoa utaratibu wa mawasiliano. Afisa wa polisi anapozungumza na mwenzake watatumia lugha yao kama inavyotumiwa kuwatambulisha. Afisa huyo huyo wa polisi anapozungumza na mshukiwa atabadilisha namna ya kuzungumza na pia anapowasiliana na mteja aliyekuja kuripoti jambo fulani pia atazungumza kwa namna tofauti. Utaratibu wa mawasiliano huelekezwa na uhusiano wa wazungumzaji.

Kanuni hizi za Halliday ni muhimu kwetu tunapobainisha sajili hii ya maafisa wa polisi. Katika sajili ya maafisa wa polisi, kanuni hizi zimesaidia katika kutambua ni kwa nini maafisa wa polisi huwasiliana kwa njia fulani wanapokuwa wenyewe na wanapokuwa na raia wengine katika kituo cha polisi.

Sajili ya maafisa wa polisi inaweza tu kutambuliwa wanapokuwa katika muktadha wao wa kazi katika kituo cha polisi. Hii ni kwa sababu, katika kituo cha polisi wapo pale kwa shughuli rasmi ya utendakazi wao. Washukiwa hufikishwa katika kituo cha polisi, walio na shida mbalimbali huja kuripoti katika kituo cha polisi na pia maafisa wa polisi wanapokuwa katika kituo cha polisi hushughulika na shughuli rasmi. Kwa hivyo, sajili ya maafisa wa polisi wanapokuwa kituoni itatambuliwa kwa msamiati maalum. Msamiati huu maalum unatusaidia katika kuchanganua na kuieleza sajili ya maafisa wa polisi.

### 2.3.1 MIFANO YA SAJILI

Katika sehemu hii, tumeonyesha baadhi ya mifano ya sajili iliyoandikwa na wanaisimu mbalimbali. Mifano hii imetuwezesha kujenga msingi wa sajili ya maafisa wa polisi.

Linda na Wareing (1999: 143) wanaeleza kuhusu sajili ya kikundi cha watu wanaoishi mtaani huko New York kama ilivyoelezwa na William Labov (1972c). Hiki ni kikundi cha watu ambao wanarandaranda mitaani na hawana makao rasmi. Nchini Kenya wanajulikana kama *chokora*. Wanasema kuwa Labov alipata kuwa wanakikundi hiki walikuwa na tabia sawa za kiisimu. Wote walitumia Kiingereza cha waamerika weusi kisicho sanifu. Wanaendelea kusema kuwa, katika kikundi hiki, kulikuwepo na vijana ambao walionekena kuwa na usemi zaidi kuwaliko wenzao. Vijana hawa walichukuliwa na wenzao kuwa watu wa kimsingi katika kikundi hiki na kwa hivyo, usemi wao ndio ulionekana kuwa wa muhimu. Vijana hawa wa kimsingi waliweza kutumia lugha hii ya kienyeji kwa uthabiti zaidi kuwaliko wenzao. Labov pia alipata kuwa namna vijana hawa walihusishwa katika lugha ya kienyeji ndivyo walivyozidisha umahiri wao wa kuzungumza kwa kutumia Kiingereza cha waamerika weusi kisicho sanifu. Wanasema kuwa kitu kilichotambulisha vijana katika kikundi hiki kama wa kimsingi, ni lugha ambayo walitumia. Wale waliotumia lugha sanifu walichukuliwa kuwa vijana wa pembeni na si wa kimsingi.

Katika sajili hii, tunaona kuwa vijana hawa wa mitaani walipunguza mipaka yao ya usemi ili kuweza kutambuliwa kama kijana wa kimsingi katika kikundi hiki. Ingawa, vijana wa kimsingi hawakutumia lugha sanifu, wale wa pembeni walitumia lugha hiyo hiyo ili kuweza kutambuliwa kama kijana wa kimsingi jambo ambalo ni la kifahari kwao. Utafiti huu wa Labov unaonyesha

kuwa, watu wa kikundi fulani hutumia lugha kwa namna moja licha ya kuwa wanavunja kanuni za lugha husika.

Sajili hii ya vijana wa mitaani ni muhimu kwetu. Tunapata kuwa vijana hawa waliweza kupunguza mipaka ya kiusemi baina yao ili kuweza kujitambulisha na kikundi husika. Maafisa wa polisi pia ni kikundi cha kijamii ambacho kinaweza kutambulishwa kwa kutumia aina ya lugha wanayoitumia. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na wetu kwa kuwa sisi tunachunguza maafisa wa polisi na tunajikita katika matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Linda na Wareing (1999: 144) pia wanaangazia utafiti uliofanywa na Eckert Penalope miaka ya 80. Hapa wanaonyesha kuwa matumizi ya lugha huweza pia kuhusishwa na mitindo ya mavazi wanayovalia watu, mtindo wa kunyoa na aina ya muziki ambao watu wanapenda. Wanaonyesha kuwa, Penalope alichunguza wanafunzi wa shule ya upili viungani mwa mji wa Detroit.

Penalope alipata kuwa katika shule ya upili, kulikuwa na makundi mawili ya kijamii: wanafunzi waliojihusisha na shughuli mbalimbali za shule kama vile michezo na uigizaji, wangejiunga na vyuo mbalimbali baada ya kukamilisha shule ya upili. Hawa walijitambulisha na kutambuliwa kwa jina la utani *jocks.* Wanafunzi ambao hawakujihusisha na shughuli za aina hii, walijiunga na kazi za mikono huko mashinani, walitambuliwa na kujitambua kama *burnouts.* Wanafunzi waliovunja ungo; wavulana kwa wasichana walitambuliwa katika makundi haya. Hata hivyo, anasema kuwa kuna wale wanafunzi ambao hawakuwa katika mojawapo wa makundi haya. Hawa walikuwa tu vuguvugu.

Penalope kama alivyonukuliwa na wanaisimu hawa wawili anasema kuwa, tabia za kiisimu ziliweza kujitokeza kwa makundi haya. Wale wanafunzi waliojihusisha na shughuli mbalimbali za shule walitumia lafudhi ya tabaka la juu ilhali wale wengine walitumia lafudhi ya kienyeji. Utafiti huu wa Penalope ni muhimu katika utafiti wetu. Katika nadharia ya maafikiano ya Giles, tunaelezwa kuwa ili watu binafsi waweze kutambulishwa na kikundi fulani cha kijamii, ni sharti kupunguza mipaka ya usemi baina yao. Katika utafiti wetu, tunachunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili ya maafisa wa polisi. Maafisa wa polisi wana malengo ya kulinda na kutekeleza sheria kinyume na wanafunzi walio na maazimio tofauti. Wanafunzi wengine kama anavyosema Penalope walijiunga na vyuo mbalimbali, wengine walifanya kazi za mikono baada ya masomo, lakini maafisa wa polisi wana kazi tayari, na wana maazimio sawa. Kwa sababu hii, utafiti wetu unabainisha matumizi ya lugha ya Kiswahili ya maafisa wa polisi.

Wardhaugh (1986: 246) anasema kuwa, muktadha na utaratibu wa mawasiliano ni muhimu. Anatoa mfano wa sajili ya Malkia. Anasema kuwa ujumbe wa Malkia wakati wa krismasi hukitwa katika muktadha na hutolewa kwa utaratibu mwafaka kama ilivyo ule wa Rais wa Amerika wa kongamano la pamoja la kitaifa la kila mwaka. Wardhaugh anasema kuwa aina ya usemi unaotolewa huwa mwafaka katika hali fulani na huweza kuwa si mwafaka katika hali nyingine tofauti. Aina fulani ya mazungumzo huwa mwafaka katika muktadha fulani. Hata hivyo, washiriki wana hiari ya kubadilisha namna ya kuwasiliana kadri wanavyobadilisha shughuli waliyokuwa wakifanya.

Utafiti huu wa Wardhaugh una kipengele muhimu kwetu. Kipengele hiki ni hiari ya kubadilisha namna ya kuwasiliana na hata ujumbe unaotolewa pindi unapobadilisha mazingira. Utafiti wetu

unachunguza namna maafisa wa polisi huwasiliana wao wenyewe na namna huwasiliana na wateja wao. Maafisa wa polisi wanapozungumza wenyewe hutumia lugha kwa namna tofauti na wanapozungumza na wahalifu na wateja wengine. Raia waliofika kuripoti kisa fulani huwasiliana na maafisa wa polisi kwa njia ya upole na huhitajika kueleza kila kitu. Maafisa wa polisi wanapowasiliana na washukiwa hubadilisha sauti yao na hapa huonyesha amri na kudhihirisha mamlaka. Hii ndio maana tunasema kuwa utafiti huu unatufaa si haba.

Spolsky (1998: 34) anachunguza sajili ya watu wa familia moja. Anajikita katika muktadha wa nyumbani. Anasema kuwa njia muhimu ya kupambanua hali ya kijamii ni kuziainisha katika sifa tatu bainishi: mahali, majukumu ya uhusiano na mada. Njia hizi tatu anaziona kama kanuni. Kanuni mojawapo anasema kuwa ni nyumbani. Anaendelea kusema kuwa kanuni kwa kawaida hupewa jina kulingana na mahali au shughuli inayoendelea mahali hapo. Katika utafiti wake, mahali ni nyumbani. Majukumu ya uhusiano yanayohusishwa na nyumbani ambayo yanahusisha familia yaani, baba, mama, watoto na wageni wanaofika. Anasema kuwa katika muktadha wa nyumbani, mada zinazozungumziwa zinahusu shughuli za familia hiyo, kuwahusu wanajamii wengine, vyakula na vifaa vya nyumbani. Aina fulani ya mazungumzo ni mwafaka katika kanuni hii ya nyumbani. Katika familia ambapo wanafamilia wanajua zaidi ya lugha moja, basi watatumia lugha tofauti kuelezea mambo tofauti.

Katika majukumu ya uhusiano, wanafamilia hutumia lugha tofauti kuonyesha uhusiano wao. Anatoa mfano wa mume na mke ambao anasema kuwa wanapowasiliana wanaweza kutumia lugha moja katika mazungumzo yao lakini baba anapozungumza na wanawe atumie lugha tofauti. Hii ni kutokana na kuwa mume na mke wana uhusiano ulio tofauti na ule wa baina ya

watoto na baba yao. Watoto na baba yao wana mipaka wanapozungumza na kwa hivyo hutumia lugha ambayo itakuwa mwafaka.

Spolsky anasema kuwa kanuni nyingine ni kazi. Mahali panaweza kuwa kiwandani, afisi au ghala. Majukumu ya uhusiano yanahusisha; mkubwa wao, wafanyakazi, washiriki, wateja, msimamizi, kastoma, na kadhalika. Mada itakayotawala inahusiana na kazi husika.

Spolsky anaonyesha kuwa wakati wa mawasiliano baina ya watu mbalimbali wa jamii, wazungumzaji hutumia aina ya lugha ambayo ni mwafaka kulingana na uhusiano wao. Katika kanuni ya kazi pia anaonyesha kuwa uhusiano ni muhimu katika uteuzi wa lugha itakayotumika. Hii inaonyesha kuwa washiriki katika mazungumzo huchagua sajili watakayoitumia ili kuonyesha uhusiano wao.

Maoni haya ya Spolsky ni muhimu kwetu. Kwa sababu katika utafiti wetu, tunachunguza sajili ya maafisa wa polisi wanapozungumza na washukiwa, waliokuja kuripoti na wanapozungumza wenyewe. Kinachojitokeza hapa ni wazi kuwa uhusiano huelekeza aina ya sajili itakayotumika katika mawasiliano. Maafisa wa polisi wanapozungumza na wenzao watatumia sajili tofauti na wanapozungumza na washukiwa.

Ili maafisa wa polisi waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo, ni muhimu kuzingatia umoja na ushirikiano kwa kila hali. Umoja katika kikundi cha kijamii ni kani muhimu ambayo ina athari katika sajili itakayotumika. Kani hii inawezesha wanakikundi kuafikiana katika sajili

wanayoitumia ili kuwawezesha kuafikia malengo yao. Kutokana na umoja huu unaodhihirika katika jamii ya maafisa wa polisi, inatuwezesha kufanya uchunguzi ili kubainisha sajili yao.

Sajili za wanaisimu hawa zimetuwezesha kuweka msingi wa utafiti wetu ambao unahusu sajili ya maafisa wa polisi. Jambo linalojitokeza ni kuwa muktadha wa mazungumzo na uhusiano wa washiriki katika mazungumzo ni mambo muhimu katika uteuzi wa sajili itakayotumika. Muktadha ni muhimu kwa kuwa huelekeza mada zitakazozungumziwa. Katika muktadha wa kituo cha polisi mada zitahusiana na shughuli za kutekeleza majukumu yao, changamoto ambazo maafisa wa polisi wanapitia na pia kuhusiana na usalama wa nchi. Uhusiano huwezesha washiriki kuteua sajili watakayotumia kutegemea na anazungumza na nani na wapi.

Katika kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi matumizi ya lugha yao hayawezi kuepukwa. Katika utafiti wetu, tunajikita katika lugha ya Kiswahili.

## 2.4 LUGHA YA KISWAHILI

Katika utafiti wetu tunachunguza sajili ya maafisa wa polisi kwa kujikita katika lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inakuwa ya kimsingi ila wanapochanganya ndimi tumeonyesha sababu ya wao kufanya hivi. Hii ni kwa sababu lugha ya maafisa wa polisi inahusishwa na kuchanganya ndimi. Ingawa hivi kuna lugha ambayo hutawala na ndio maana tunajikita katika lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Mukhwana (1990: 1) lugha haiwezi kutenganishwa na jamii, maana mahusiano ya kilugha ni mahusiano ya kijamii vilevile. Anaendelea kusema kuwa, kuchagua lugha fulani itumike mahali fulani na watu fulani hufanywa ili kuathiri muundo wa jamii husika ili

kutosheleza mahitaji fulani ya kijamii. Hii ina maana, jamii hutumia lugha fulani katika muktadha ambao unaruhusu aina hiyo ya lugha kutumika. Wazungumzaji hutumia aina fulani ya lugha kwa nia fulani.

Maafisa wa polisi huwasiliana kwa kutumia lugha baina yao na pia wao na wateja au na washukiwa. Aina ya lugha itakayotumiwa baina yao ni tofauti na ile wanayozungumza na washukiwa. Maafisa wa polisi wanapozungumza na wanaokuja kuripoti jambo fulani hutumia lugha ya upole ili kuweza kupata ujumbe wote unaohitajika, lakini, wanapozungumza na washukiwa, hutumia lugha ya amri na hutaka washukiwa hawa kutekeleza mambo fulani bila kusita.

Nafasi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya ni jambo la kimsingi kwa watumizi na matumizi ya lugha hii. Hii ndio lugha ya taifa. Lugha ya taifa ni lugha ambayo imepewa hadhi na kupewa jukumu la kutumiwa na watu wa taifa fulani. Kwa mujibu wa Iribemwangi na Mukhwana (2011: 103) taifa ni kikundi cha watu wanaojitambulisha na chimbuko au usuli mmoja. Watu hawa huwa na historia moja na ndio maana wanachukuliwa na kujichukulia kuwa kitu kimoja. Basi, lugha ya taifa ni lugha inayotumiwa na watu wa taifa fulani. Lugha hii hutumiwa kuwaunganisha watu wa taifa hilo. Ili lugha iweze kupewa hadhi ya kuwa lugha ya taifa, huwa imevuka mipaka ya kikabila na inapaswa kutumiwa na watu wote kama njia ya kuwasawazisha.

Mukhwana (2008: 2) anasema kuwa Kenya ilipojinyakulia uhuru mwaka wa 1963, Kiingereza kilifanywa kuwa lugha rasmi na Kiswahili kikapewa hadhi ya kuwa lugha ya kitaifa. Lugha hizi mbili zinatumiwa katika mawasiliano nchini Kenya. Anasema kuwa, hata hivyo, watu wengi

wanaweza kuzungumza Kiswahili au Kiingereza au zote. Rais wa Kenya wa wakati huo Mzee Jomo Kenyatta alitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa. Ingawa tangazo lake halikuwekwa katika maandishi wananchi waliendelea kukitumia Kiswahili kama lugha sawazishi.

Kiswahili kama lugha ya taifa hutumiwa wakati wa maingiliano baina ya watu mbalimbali. Kiswahili kinatumika kwingi na katika katiba mpya ya mwaka 2010, kimepewa hadhi ya kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza. Katika kituo cha polisi cha Central, Kiswahili hutumika sambamba na lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, mazungumzo hutawaliwa na lugha ya Kiswahili kisha kuchopeka lugha ya Kiingereza hapa na pale.

Whiteley (1974: 190) anadai kuwa katika mahusiano baina ya watu mbalimbali, mawasiliano huanza kwa namna fulani kisha kunatokea mabadiliko kadri wanavyoendelea kuwasiliana ili kuweza kuafikiana. Ukurasa wa 208 anasema kuwa Kiingereza hutumiwa na vijana walioelimika zaidi kuliko vijana ambao wana elimu kiasi tu. Anaendelea kusema kuwa, Kiswahili hutumiwa na watu wa matabaka yote, lakini zaidi na wale wa tabaka la chini.

Whitely anaendelea kusema kuwa watu wanapokutana kwa mara ya kwanza, huzungumza kwa kutumia Kiswahili mwanzo kabisa kisha kutakuwepo na kubadili lugha hadi kwa Kiingereza au lugha za kienyeji. Kubadili lugha katika mawasiliano kutoka Kiswahili hadi Kiingereza hutegemea na uhusiano wa washiriki wa mazungumzo hayo.

Maafisa wa polisi  hukumbana na watu kutoka matabaka mbalimbali na walio na viwango tofauti vya elimu.  Kutokana na maoni ya Whiteley ni wazi kuwa mteja anapofika katika kituo cha

polisi ataanza kuzungumza kwa Kiswahili. Kadri wanavyoendelea kuzungumza ndivyo wanaendelea kuafikiana katika mazungumzo na kwa hivyo wanaweza kutumia Kiingereza hapa na pale. Hapa tunapata kuwa, Kiswahili ni lugha ya kimsingi katika mawasiliano na ndio sababu tunajikita kwacho.

Katika sura hii, tumeonyesha dhana muhimu katika utafiti wetu na namna tunavyozitumia. Tumeonyesha aina za sajili mbalimbali ambazo zimeshughulikiwa na wanaisimu mbalimbali kama njia ya kujenga msingi wa kazi yetu. Pia, tumeonyesha kuwa tunajikita katika lugha ya Kiswahili. Ili kuweza kuangazia namna tunavyotumia dhana hizi na lugha ya Kiswahili katika utafiti wetu tunachanganua data kwa mujibu wa nadharia tunazozitumia katika sura zinazofuata.

# SURA YA TATU

# MISIMBO NA MAAFIKIANO KATIKA SAJILI YA MAAFISA WA POLISI

## 3.0UTANGULIZI

Katika Sura ya Pili, tumebainisha maana ya dhana muhimu katika utafiti wetu. Pia, tumetoa baadhi ya mifano ya sajili ambazo zimeweza kubainishwa na wataalamu mbalimbali. Tumeangazia sifa za sajili hizi kwa kuwa zinatuwezesha kujenga msingi wa kazi yetu.

Katika sura hii, tunajikita katika nadharia za Bernstein (1971) ya misimbo na nadharia ya Giles (1987) ya maafikiano. Nadharia hizi zinatuwezesha kuchunguza na kubainisha mazungumzo baina ya maafisa wa polisi wenyewe. Tumebainisha namna maafisa wa polisi hutumia lugha ya Kiswahili katika sajili yao.

Nadharia ya Bernstein ya misimbo inaonyesha kuwa matumizi ya lugha ya kila siku huakisi na huonyesha hali halisi ya chukulizi kuhusu utambulisho wa kikundi fulani. Kikundi husika huweza kuathiri matumizi ya lugha ya mtu binafsi ili aweze kutambuliwa katika kikundi hicho. Bernstein anachukulia lugha kama kaida zilizoidhinishwa ambapo misimbo ya usemi hutumika.
Nadharia ya msimbo inatuwezesha kubainisha aina ya msimbo ambao maafisa wa polisi hutumia. Tunaangazia aina mbili za msimbo: msimbo pana na msimbo finyu. Maswali tunayojiuliza ni:

a. Je, maafisa wa polisi wanapozungumza wenyewe hutumia msimbo finyu au pana?
b. Wao hutumia msimbo upi, wapi na lini?

Ubainishaji huu wa misimbo wanayoitumia unatuelekeza hadi kwa maafikiano. Katika isimujamii, utafiti wa lugha huvuka sentensi zinazotolewa kwa kueleza na kubainisha sifa za sajili ya maafisa wa polisi. Muktadha wa uhusiano wa wanajamii huwa muhimu. Maafisa wa polisi kama kikundi cha kijamii wana sajili yao ambayo inaweza kutambuliwa. Kwa sababu hii, kuna sifa ambazo zinatumiwa kuonyesha kuwa wao ni kikundi cha kijamii.

### 3.1.1.0 MSIMBO PANA

Katika msimbo pana, wazungumzaji huzungumza mambo yote wazi kwa sababu ni muhim kila mshiriki aelewe kinachosemwa. Hali za mazungumzo au mada ndizo huwafanya wazungumzaji kutumia aina hii ya mazungumzo. Msimbo pana huibuka kutegemea uhusiano wa wazungumzaji. Uhusiano baina ya wazungumzaji ni muhimu kwa kuwa huwawezesha kuteua msamiati ambao utaeleweka na washiriki wote. Mzungumzaji hutilia maanani hali ya msikilizaji na hii huchochea mzungumzaji kusema kila kitu wazi bila kubana.

Katika sajili ya maafisa wa polisi, msimbo pana hutumika pale ambapo wanazungumzia mambo ya kijumla, yaani, mambo ambayo yanahusu maisha ya kila siku, kama vile, elimu, michezo, siasa na mambo mengine. Haya ni mambo ambayo hayahitaji kubanwa kwa kuwa hayana siri yoyote. Mazungumzo haya aghalabu huwa wakati ambao wanapumzika kituoni hasa wanapokuwa katika duka lao lililo hapo kituoni. Wazungumzaji wanaweza kutumia msimbo pana kwa sababu kadha:

### 3.1.1.1 KUTOA HISIA

Wazungumzaji huwasilisha hisia zao kwa njia wazi. Maafisa wa polisi wanapozungumzia mada fulanifulani wanatoa hisia zao. Katika baadhi ya mada wanazozungumzia maafisa wa polisi ni siasa na wanasiasa. Siasa na wanasiasa huchangia katika uchumi wa nchi. Uchumi wa nchi huwa na athari kwa wananchi. Ukosefu wa amani huchangia katika kudorora kwa uchumi. Wanasiasa wana uwezo wa kudumisha au kukomesha ghasia tunazokumbana nazo. Wanasiasa wana uwezo wa kubadilisha uchumi wa nchi.  Maafisa wa polisi wanapozungumza kuhusu siasa, huzungumza wazi bila kubana. Maafisa hawa huzungumza huku wakidhihirisha hisia zao wazi.

Mfano 1:

Afisa 1: Ukweli hatuogopi Raila,

Afisa 2: Lakini hapana, unaona 2017, Raila atachukua vile Kibaki alichukua.

Sikudanganyi, Raila atachukua.

Afisa 3: Mmmh, na akichukua atasafisha ile ghasia yote imetokea kwa hii nchi?

Maafisa hawa watatu wa polisi wanazungumzia siasa. Katika mazungumzo yao, wanataja kila jambo waziwazi. Majina ya wanasiasa yanatajwa wazi na pia kila mmoja anasema hisia zake bila kuficha. Siasa wanazozungumzia hazitatizi usalama wa nchi, ndio maana wanasema mambo yote wazi.

Raia yeyote anaweza kufuatilia mazungumzo haya. Mazungumzo haya yanawahusu wanasiasa maarufu na ambao wamewahi kuongoza taifa hili. Wananchi wanajua sifa zao ila kila mmoja huwa na mtazamo tofauti kuwahusu na kuhusu uongozi wao. Maafisa hawa wa polisi wanapozungumza kuhusu siasa na wanasiasa wanaelezea hisia zao ambazo hazifichiki ndiposa

wanazungumza wazi. Hisia za mtu hazifichiki ndiposa wanazungumzia mambo wazi bila kuzingatia hisia za washiriki wengine. Kila mmoja wao anasema anachofikiria bila kubana.

Maafisa wa polisi pia wanapozungumzia mambo ya pesa na malipo huzungumza wazi. Maafisa wa polisi hulipwa kati ya tarehe ishirini na thelathini. Kutokana na kuzoea malipo ya mapema, mshahara ukicheleweshwa wao hukerwa na hulalamika. Malalamishi yao yanaonyesha hisia zao. Kwa mfano,

Mfano 2:

Afisa 1: Sasa hii pesa itaingia lini jameni?

Afisa 2: Hata hawajatengeneza payroll.

Afisa 1: Imekuwa official, wacha wakae nayo kama hawataki.

(payroll- orodha ya kulipa mshahara)

(official- ni rasmi)

Hisia zinazotolewa hapa ni za kutoridhishwa na kucheleweshwa kwa mshahara wao. Afisa 1 anaposema kuwa "Wacha wakae nayo kama hawataki" inaonyesha kuwa wamechoka kusubiri. Maafisa wa polisi wanataja mambo yote wazi. Mambo yanayohusiana na pesa hayana siri katika mazungumzo yao. Katika mazungumzo haya hisia zinazotolewa ni za hasira ya kutolipwa kwa wakati waliozoea. Maafisa wa polisi wanapotoa hisia za kuonyesha hasira hutaja mambo yote wazi kwa kutumia msimbo pana. Hii ni kwa sababu, wanapokerwa na jambo fulani, hawana muda wa kuteua msamiati ambao unaficha wanayoyazungumzia. Maafisa wa polisi wanapotoa hisia zao hutumia msimbo pana. Hii ni njia mojawapo ya maafikiano kwa kuwa washiriki katika mazungumzo hutumia msimbo pana.

### 3.1.1.2 RAI

Rai ni kumwomba mtu afanye jambo fulani bila kumkemea. Mzungumzaji anapotoa rai hana haja ya kuficha anachokisema. Kinyume na ilivyo wakati wa kutoa amri katika mazungumzo baina ya maafisa wa polisi, rai hutolewa kwa njia wazi bila kubana mambo mengine. Kwa mfano;

Mfano 3:

> Afisa 1: Nanii bwana, wewe naomba uwache kuruka kazi. Hata wewe ukitoka nyumbani, si hata bibi anajua kuwa uko Nairobi unafanya kazi.
>
> Afisa 2: Hunielewi afande.

Haya ni mazungumzo baina ya afisa wa polisi ambaye ni koprol na afisa mdogo wake. Afisa huyu wa polisi ana mazoea ya kutofika kazini anavyotakiwa. Jambo hili limemkasirisha koprol. Koprol anaamua kumwonya afisa huyu wa polisi kwa kumrai awe kazini kulingana na ratiba. Koprol anapotumia neno ‘Naomba’ anamsihi afisa huyu wa polisi.

Koprol anatumia maneno wazi kwa afisa wa polisi aliye mdogo wake kikazi kwa kuwa hatumii sheria ya kuwaadhibu maafisa wa polisi wasiofika kazini kama wanavyotakiwa. Maafisa hawa wa polisi wanakuwa na mlahaka mzuri na afisa anakubali kumweleza koprol changamoto anazozipitia ambazo zinamfanya asifike kazini anapotakiwa kuwepo.Uhusiano unajengeka baina yao ingawa afisa wa polisi katika kiwango cha koprol ni mkubwa wa afisa huyu wa polisi. Uhusiano huu unawafanya kuwa kama walio katika kiwango kimoja ndiposa afisa wa polisi anamweleza koprol changamoto anazozipitia zinazomfanya asifike kazini ilivyoratibiwa.

Mazungumzo haya ya maafisa wa polisi yanadhihirisha matumizi ya msimbo pana. Hii ni kwa sababu mada wanazozizungumzia hazitatizi usalama wa nchi. Wanazungumza mambo yao ambayo wanayajua na wanayoyafikiri kwa kutumia maneno yanayoeleweka na washiriki wote.

Katika mazungumzo ya maafisa hawa wa polisi, mambo yamezungumzwa wazi bila kubana ujumbe. Mazungumzo yao yanaonyesha kuwa hakuna aliyekuwa na ujumbe unaozungumziwa hapo kimbele. Kila kitu kinasemwa wazi ili kuendeleza mazungumzo na pia kwa nia ya kutaka kujua zaidi. Washiriki wote wanaelewa kinachosemwa. Mambo yaliyokuwa yamejulikana kimbele huwatenga watu wasiokuwa katika kikundi hiki. Mada hizo tunazijadili katika sehemu inayofuata.

### 3.1.2.0 MSIMBO FINYU

Msimbo finyu hutokea pale ambapo wazungumzaji wanajua kuhusu jambo fulani kimbele. Msikilizaji ambaye hana habari hiyo hawezi kuelewa mazungumzo hayo. Maafisa wa polisi wanapozungumzia mambo yanayohusu usalama wa wananchi hutumia msimbo finyu ili kutenga makundi mengine ya kijamii. Hatujaangazia mifano mingi kwa kuwa mambo ya usalama nchini ni swala nyeti na tete. Wanakikundi husema kile wanachotaka kukisema kwa kubana wanayoyazungumzia kwa sababu mbalimbali.

### 3.1.2.1 UFAHAMU WA AWALI

Maafisa wa polisi wanapotumia msimbo finyu huashiria umoja wao. Hii huonyesha kuwa wao ni kikundi kimoja ambacho kina utaratibu wa kutoa mawasiliano huku wakidhihirisha kuwa wana habari za kimbele kuhusu wanachokizungumzia. Maafisa wa polisi wanapozungumzia mambo yasiyowahusu watu wengine waliopo kwenye kundi hilo hutumia msimbo finyu. Kwa mfano,

Mfano 4:

Afisa 1: OC nani yeye?

Afisa 2: Ni wale wasumbufu tu.

Afisa wa polisi 2 ambaye anatuongoza anaulizwa na mwenzake kuwa mimi ni nani baada ya kuniona nimeketi karibu nao. Kiongozi wetu alikuwa amemweleza hapo mbeleni kuwa mimi ni mtoto wa dadake na huja kudai pesa kila wakati. Afisa 2 anaposema kuwa ni wale wasumbufu inaonyesha kuwa walikuwa wamezungumzia jambo hili hapo awali. Afisa 1 anapoambiwa kuwa "Ni wale wasumbufu" anaelewa kinachozungumziwa na haendelei kuuliza maswali. Afisa 1 asingekuwa na habari za awali, angeendelea kuuliza maswali kwa kutaka maelezo zaidi.

#### 3.1.2.2 SIRI

Maafisa wa polisi wana njia yao ya kuficha siri ili asiyekuwa mmoja wa kikundi chao asielewe kinachosemwa. Mawasiliano ya maafisa wa polisi yamesheheni siri ili wasije wakaharibu mambo. Wamebuni namna ya kutaja sauti zao za konsonanti na irabu. Kwa mfano,

Mfano 5:

Afisa 1: Huyu ni ule…….

Afisa 2: Ni Romeo, Uniform, Tango, Hotel.

Afisa 1. Singemtambua kabisa. Amebadilika leo au ni nguo imembadilisha?

Afisa 1 alitaka kujua mimi ni nani. Afisa 2 hakutaka kulitaja jina Ruth wazi kwa kuwa hakutaka nijue kama ndimi waliokuwa wakizungumza kunihusu. Maafisa hawa wa polisi wanaamua kutumia majina ambayo wao hutumia kutajia sauti fulani: Romeo ni sauti R, Uniform ni sauti U,

Tango ni sauti T na Hotel ni sauti H, sauti hizi zinaunda jina *Ruth* baada ya kuchukua herufi za mwanzo. Mfano mwingine kama huu ni,

Mfano 6:

Afisa 1: Amenileta juujuu.

Afisa 2: Huyo India Papa.

Afisa 3: Hei, tangu awe hapo anatutesa kweli, lakini ni sawa tu.

Maneno *India Papa* ni maneno ya kuficha siri. India kama tunavyojua ni nchi na Papa ni aina ya mnyama wa baharini. Katika mazungumzo haya wanazungumzia Inspekta wa Polisi (IP).

Mifano hii miwili inaonyesha namna ambavyo maafisa wa polisi wanavyoficha siri zao. Maafisa wa polisi wanapotumia majina fulani kurejelea sauti fulani ni kutenga makundi mengine ya kijamii. Katika mawasiliano yao wanaruhusiwa kutumia sauti kwa njia hii ili kuweza kuficha siri hasa ikiwa wanarejelea miji, watu au hata mashirika mbalimbali yaliyo na tatizo fulani.

Msimbo finyu ni muhimu kwa maafisa wa polisi kutokana na kuwa suala la usalama ni tete mno. Hii inaashiria kuwa kikundi hiki kinadhihirika wazi kwa kuwa kina mfumo thabiti. Mfumo huu thabiti ndio huwawezesha kutekeleza majukumu yao. Maafisa wa polisi wanapowasiliana kwa kutumia msimbo finyu, wanatenga kikundi ambacho hakipaswi kujua ujumbe unaopitishwa. Msimbo finyu hutumiwa hasa wanapotaka kuwanasa washukiwa.

Tumeonyesha namna ambavyo maafisa wa polisi hutumia msimbo pana na msimbo finyu. Msimbo pana huwasaidia katika kuwasilisha hisia zao. Hisia hizi hutokana na mambo ya kawaida ya maisha kama vile siasa, elimu, gharama ya maisha na mambo mengineyo sampuli

hii. Wao huzungumzia mambo haya wanapokuwa mapumzikoni na wakati wanapopata chamcha. Huu ni wakati ambao wanapumzika na kusahau changamoto za kazi yao. Mazungumzo ya aina hii huwachangamsha na kwa sababu hii wao huzungumza wazi bila kubana.

Tumeonyesha kuwa msimbo finyu hutumiwa zaidi wanapozungumzia mada zinazohusu usalama. Usalama wa nchi ni jambo tete hasa kutokana na mashambulizi ya mara kwa mara. Hii ndio maana wao hutumia msimbo finyu ili raia wasije wakagundua siri zao. Ni muhimu kwa maafisa wa polisi kuzungumzia mambo yanayohusu usalama kwa kutumia msimbo finyu hasa maneno wanayoyajua wao wenyewe ili raia wasije wakaelewa yale wanakusudia kutenda. Ni kutokana na ukweli huu ndiposa hatungeweza kuzungumzia mengi kuhusu msimbo finyu tusije tukahujumu usalama.

Kufikia kiwango hiki, ni vizuri kuonyesha sifa ambazo hutambulisha maafisa wa polisi kama kikundi cha kijamii. Maafisa wa polisi wana sare rasmi ambazo huwatambulisha ila pia wanaweza kutambuliwa kutokana na matumizi yao ya lugha. Hii ndio sababu tunahitaji nadharia inayofuata.

## MAAFIKIANO KATIKA SAJILI YA MAAFISA WA POLISI

### 3.2.0UTANGULIZI

Sehemu iliyotangulia na sehemu hii zina mwingiliano. Katika sehemu hizi mbili, tunashughulikia sajili ya maafisa wa polisi wanapokuwa wakizungumza wenyewe. Katika sehemu iliyotangulia, tumeangazia misimbo. Tumechanganua data kwa msingi wa nadharia ya Bernstein ya misimbo. Tulianza na misimbo kwa nia ya kuonyesha namna maafisa wa polisi huwasiliana kutegemea na uhusiano baina yao. Hii ni njia mwafaka ya kujenga msingi katika sehemu hii inayohusu maafikiano.

Katika sehemu hii, tunajikita katika nadharia ya Giles ya maafikiano. Mtu binafsi huzungumza kama washiriki wa kikundi alicho (Giles 1975: 155). Anasema kuwa hii inaashiria kuwa kuna mtazamo chanya wa washiriki wa kundi hilo kuhusu kazi yao. Nadharia hii inashikilia kuwa mshiriki wa kikundi fulani cha kijamii hupunguza mipaka baina yake na washiriki wengine wa kundi hilo kwa nia ya kuafikiana. Maafikiano haya hutokea ili kuweza kudumisha uhusiano baina yao hasa wanapokuwa katika muktadha fulani maalum. Muktadha rasmi wa maafisa wa polisi ni katika kituo cha polisi. Maafisa wa polisi wanapokuwa katika kituo cha polisi hudhihirisha kundi lao la kijamii kupitia kwa matumizi yao ya lugha.

Giles (1975: 158) anasema kuwa, maafikiano katika usemi yanaweza kuchukuliwa kama jaribio la mzungumzaji kubadili usemi unaomtambulisha yeye kama mtu binafsi na kusema kama washiriki wa kundi hilo. Mabadiliko haya hutokea bila ya hiari ya msemaji.

Kikundi cha maafisa wa polisi huwa na watu waliotoka jamiilugha mbalimbali. Maafikiano baina yao yanaweza kudhihirika katika mazungumzo baina yao wanapotumia lugha ya Kiswahili. Katika utafiti wetu, tuligundua kuwa maafisa wa polisi wanaweza kuwasiliana kwa kutumia lugha ya Kiswahili, lakini, wanapokitumia Kiswahili, wao huchopeka maneno ya lugha ya Kiingereza au lugha zao za kwanza hapa na pale.

Katika sehemu hii, tunaangazia namna maafisa wa polisi huwasiliana kwa kujikita katika lugha ya Kiswahili. Tumeangazia sifa za mazungumzo yao ambazo zinaashiria uwepo wa maafikiano baina yao.

### 3.2.1.0 KUCHANGANYA NDIMI

Kuchanganya ndimi ni hali ambapo wazungumzaji wanatumia lugha tofauti katika mazungumzo yao kwa muda tofauti. Wazungumzaji wanaweza kutumia lugha zaidi ya moja katika sentensi moja na wanaweza kufanya hivyo mara kadha. Aina hii ya kuchanganya ndimi mada haibadiliki, lakini, pia kuna aina nyingine ya kuchanganya ndimi ambapo wazungumzaji huchanganya ndimi kadri mada inavyobadilika.

Wardhaugh (2002: 102) akimnukuu Gal anasema kuwa kuchanganya ndimi ni mkakati mojawapo wa kuunganisha au kuharibu mipaka ya kikundi; ili kuunda, kuchochea au kubadilisha uhusiano baina ya wanakikundi. Maoni yake yanaonyesha kuwa kuchanganya ndimi ni njia mojawapo ya kujenga au kutenganisha kikundi. Wanakikundi wanapochanganya ndimi huweza kukuza uhusiano wao na hii huashiria maafikiano.

Maafikiano ni njia moja ya kueleza namna mtu binafsi na kikundi husika wanavyohusiana. Kuchanganya ndimi ni hali ya kuonyesha ushirikiano. Ushirikiano huu hudhihirisha kuwa mshiriki fulani anatilia maanani hali za washiriki wengine wa kikundi hicho na hii huonyesha maafikiano. Maafisa wa polisi kama kikundi cha kijamii, wanapochanganya ndimi hudhihirisha maafikiano baina yao.

Katika kuchanganya ndimi, lugha moja ndio hutawala mazungumzo ila panakuwa na uchopekaji wa maneno ya lugha nyingine hapa na pale. Katika mazungumzo baina ya maafisa wa polisi, lugha ya Kiswahili hutawala mazungumzo huku wakichopeka maneno ya Kiingereza hapa na pale. Katika sajili ya maafisa wa polisi, kuchanganya ndimi ni jambo linalotokea mara kwa mara katika mazungumzo baina yao. Maafisa wa polisi huchanganya ndimi kwa sababu mbalimbali.

#### 3.2.1.1 KUJIELEZA VIZURI

Lugha ya Kiswahili inakua, kwa sababu hii, kunayo misamiati mipya ambayo huzuka kila uchao. Kwa sababu hii, wazungumzaji hutumia maneno ya Kiingereza yaliyozoeleka. Kwa mfano,

Mfano 7:

Afisa 1: Hiyo ni automatic.

Afisa 2: Wee, sikiliza nikueleze, you have said your mind. Kitu mimi naweza kusema hata kama ni nani hii serikali hataiweza.

Afisa 3: Katiba ndio mbaya, ikifanyiwa amendment, viongozi watawajibika.

( Automatic- wazi)

(You have said your mind- umesema unavyofikiri)

(Amendment- marekebisho)

Mazungumzo baina ya maafisa hawa watatu yamesheheni kuchanganya ndimi. Wote watatu wanatumia lugha ya Kiswahili katika mazungumzo ila kila mmoja amepachika neno au maneno ya lugha ya Kiingereza katika usemi wake. Afisa 1 anapotumia neno *automatic* anajieleza vizuri kinyume na angetumia neno la Kiswahili wazi au dhahiri. Maneno haya ya Kiswahili yana maana ambayo si ya moja kwa moja kama ilivyo neno la Kiingereza. Afisa 2, ametumia maneno ya Kiingereza-*you have said your mind* maneno haya kwa Kiswahili ni 'umesema kile ambacho wewe unafikiria.' Maneno haya ya Kiswahili hayatokei kwa wazi kama ilivyo kwa maneno ya Kiingereza. Afisa 3 anatumia neno *amendment.* Neno hili katika lugha ya Kiswahili ni 'marekebisho' ambalo likibadilishwa kwa lugha ya Kiingereza linaweza kuwa na maana ya *correction* na hii inaleta maana tofauti na iliyokusudiwa.

Maafisa hawa wa polisi wote wanachanganya ndimi katika semi zao. Hii inaonyesha kuwa kuna maafikiano baina yao. Wote watatu wanatumia maneno ya Kiingereza ili kuweza kujieleza vizuri. Maneno ya Kiswahili yangetumika pale ambapo wamechopeka maneno ya Kiingereza basi wangezua maana zaidi ya moja. Ili kuepuka hali ya kuzua maana zaidi ya moja, wanachanganya ndimi ili kutumia maneno ambayo yataeleweka moja kwa moja.

### 3.2.1.2 KUFIDIA MSAMIATI

Maneno mengine huwa hayapatikani kwa lugha ya Kiswahili, kwa hivyo, maafisa wa polisi wanapozungumza na wahitajike kutumia maneno hayo, hulazimika kuchanganya ndimi. Maafisa wa polisi pia inawezekana wasijue msamiati mwafaka wa lugha ya Kiswahili. Neno la kuashiria kitu au jambo fulani lipo ila wao hawalijui. Maafisa wa polisi huchanganya ndimi ili kufidia

msamiati ambao haupo kwa lugha ya Kiswahili au wao wenyewe hawajui kama kuna neno mwafaka la Kiswahili. Kwa mfano,

Mfano 8:

Afisa 1: Unafaa kupitia Eastern bypass.

Afisa 2: Wewe unajua maeneo hatari. Na wale watu wa pikipiki ambao hutuletea shida na wanaopitisha masaa ya Mututho washikwe.

( Eastern bypass- barabara ya kando ya mashariki)

Katika mfano huu, neno *bypass* halina msamiati mwafaka wa lugha la Kiswahili. Afisa 1 alilazimika kulitumia kwa kuwa hakuwa na msamiati mwafaka wa lugha ya Kiswahili. Afisa 1 pia ametumia neno *Eastern* ambalo kwa Kiswahili ni Mashariki. Hata hivyo, afisa 1 analitumia kwa kuwa neno la pili, *bypass* lina uhusiano na lile la kwanza na ndio maana hangeweza kutumia neno Mashariki. Afisa huyu wa polisi angetumia neno la Kiswahili- barabara ya kando hangeeleweka kwa kuwa maana yaweza kuwa wanakopitia wanaosafiri kwa miguu au upande wa mashariki wa barabara.

Maneno mengine katika lugha ya Kiswahili huwa ya jumla kinyume na ilivyo katika lugha ya Kiingereza. Katika Kiswahili, barabara huwa neno la jumla, ilhali katika Kiingereza kuna: *way avenue, walk, street, lane* na kadhalika. Maafisa wa polisi wanapozungumza kuhusu masuala ya kufanya msako au mahali ambapo wamejulishwa kuwa kuna tatizo fulani la kiusalama katika barabara fulani, hulazimika kutumia neno la Kiingereza ili kuweza kuelewa vyema. Kwa mfano,

Mfano 9:

Afisa 1: Usimamie hapo university way.

Afisa 2: Ndio afande, nitakuwa hapo mahali Koinange street inaanzia kwa sababu wengine wanavukia hapo tu.

(University way- barabara ya chuo kikuu)

(Koinange street- barabara ya Koinange)

Afisa 2 anaelezwa ambapo anapaswa kusimama ili kutekeleza majukumu yake. Wametumia maneno ya Kiingereza kutajia barabara kwa kuwa maneno hayo ni mwafaka. Maafisa hawa wa polisi wangetaka kutumia maneno ya Kiswahili basi wangesema barabara ya chuo kikuu na barabara ya koinange. Maneno haya yangezua utata na ingemchukuwa muda anayezungumziwa kuelewa anayoelezwa.

Jambo jingine ambalo husababisha hali ya kuchanganya ndimi ni kuwa inawezekana maafisa wa polisi wanaozungumza hawajui kuwa kuna maneno ya Kiswahili ambayo yanaashiria dhana au hali wanazozungumzia. Maafisa wa polisi wanapozungumzia kuhusu usalama na viongozi wao, hulazimika kutumia maneno ya Kiingereza. Kulingana nao, yapo maneno ambayo hayapatikani katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano,

Mfano 10:

Afisa 1: Ako chini ya Chief Security Officer

Afisa 2: Na si huyo mtu alikuwa tu OCS juzi.

(OCS- Officer Commanding Station- msimamizi wa kituo)

( Chief Security Officer- Afisa mkuu wa usalama)

Maafisa wa polisi hapa wanazungumza kuhusu maafisa wengine wa polisi walio na vyeo. Maneno *Chief Security Officer* na *Officer Commanding Station*, kwa Kiswahili ni Afisa Mkuu wa Usalama na Afisa anayesimamia kituo mtawalia, hayapo katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, ingawa maneno haya yapo katika lugha ya Kiswahili, huwa yanaleta utata kidogo. Tunasema hivi kwa sababu, maneno kama vile *Head*, *Chief*, katika Kiswahili ni mkuu. Hii inaonyesha kuwa maafisa wa polisi wanalazimika kutumia maneno ya lugha ya Kiingereza kurejelea vyeo mbalimbali.

### 3.2.1.3 KURAHISISHA MAWASILIANO

Maafisa wa polisi huchanganya ndimi kwa nia ya kurahisisha mawasiliano. Maneno hasa yanayorejelea vyeo vya maafisa wa polisi huwa yanafupishwa katika lugha ya Kiingereza kwa kuchukua herufi za mwanzo za maneno husika. Maneno haya ya kurejelea vyeo hayana ufupisho wake katika lugha ya Kiswahili. Hii ndio sababu maafisa wa polisi wanapotumia maneno haya katika sentensi hulazimika kuchanganya ndimi kwa kutumia vifupisho vya lugha ya Kiingereza. Kwa mfano,

Mfano 11:

> Afisa 1: Sema OC, umepotea sana.
>
> Afisa 2: Poa, haya mambo ya Al shabaab yanatufanya hatulali. Hata IG amekonda mbaya bwana.

(OC- Officer Commanding – afisa msimamizi)

(IG- Inspector General – inspekta mkuu wa polisi)

Maneno haya katika lugha ya Kiswahili ni afisa anayesimamia kituo na inspekta mkuu wa polisi mtawalia, lakini katika lugha ya Kiswahili vifupisho vyake havijazoeleka. Maafisa hawa wa polisi wanazungumza kwa kutumia lugha ya Kiswahili lakini wanapofika katika kutaja vyeo hutumia maneno hayo kwa kifupi namna yanavyojulikana kwa lugha ya Kiingereza. Kwa kufanya hivi, maafisa wa polisi wanarahisisha mawasiliano kuliko wangetumia maneno hayo kwa lugha ya Kiswahili ambapo wangelazimika kuyataja kama yalivyo kwa kuwa ufupisho wake haujazoeleka.

Maafisa wa polisi wanapotaka kutaja vyeo katika idara yao, hutumia vifupisho. Hili ni jambo linalotokea kwa maafisa wa polisi na imekuwa ni kama mazoea. Jambo hili la kutumia maneno ya vyeo kwa kuchukua herufi za mwanzo katika maneno linadhihirisha maafikiano. Maafikiano haya yanadhihirika hata kwa walio na vyeo. Hali hii inadhihirisha kuwa kuna umoja katika kikundi hiki na maafikiano.

**3.2.1.4 MSISITIZO**

Maafisa wa polisi hutumia maneno ya Kiingereza wanapokuwa wakizungumza kwa kutumia lugha ya Kiswahili kuonyesha msisitizo. Msisitizo huwa wa maneno ambayo yana uzito fulani katika sentensi husika. Kwa kuchopeka neno la lugha ya Kiingereza, kunatokea ile tofauti baina ya maneno yanayozungumziwa. Maneno haya wanayoyataja kwa lugha ya Kiingereza huwa ni maneno yanayotumiwa kuashiria neno lenye uzito katika sentensi hiyo. Kwa mfano,

Mfano 12:

Afisa 1: Hii constitution yenyewe ni mbaya.

Afisa 2: Wacha nikuambie, wakati ile watu walichinjwa mimi nilikuwa pale. Ile kitu ilikuwa

Political.

(constitution- katiba)

(political- kisiasa)

Maafisa hawa wa polisi wametumia maneno ya Kiingereza ambayo wanajua namna yanavyotajwa katika lugha ya Kiswahili. Maafisa hawa hawakukosa msamiati mwafaka, ila wanatumia maneno hayo ya lugha ya Kiingereza ili kuonyesha maneno ambayo wanayatilia msisitizo. Kuonyesha kuwa kilicho na uzito katika sentensi ya afisa 1 ni katiba na sentensi ya afisa 2 ni kisiasa. Maneno mengine katika mazungumzo haya yametumika tu ili kuwasilisha ujumbe lakini yale ya lugha ya Kiingereza yanaonyesha mahali pa msisitizo.

Mazungumzo baina ya maafisa wa polisi yamedhihirisha hali ya kuchanganya ndimi. Maafisa wa polisi tuliorekodi wametumia Kiswahili katika mazungumzo yao ila wanachopeka maneno ya Kiingereza hapa na pale. Tumeonyesha sababu ambazo huwafanya maafisa wa polisi kuchanganya ndimi. Tumeona kuwa wao huchanganya ndimi kwa sababu wanataka kujieleza vizuri, kufidia msamiati, kurahisisha mawasiliano na pia kuonyesha maneno wanayoyatilia msisitizo. Mambo yanayoonyesha maafikiano katika kikundi hiki cha kijamii cha maafisa wa polisi.

Mifano tuliyotoa inaonyesha kuwa maafisa wa polisi wanaweza kutawala kaida za matumizi ya lugha katika mazungumzo yao. Maafisa wa polisi wametumia lugha za Kiswahili na Kiingereza katika sentensi moja na wamefanya hivyo hivyo katika mazungumzo yao. Matumizi haya ya lugha zaidi ya moja yanadhihirisha maafikiano.

### 3.3.0 SARUFI

Tunatumia neno sarufi hapa kwa maana ya matumizi sahihi ya maneno katika sentensi. Katika mazungumzo ya maafisa wa polisi, tuligundua kuwa hawazingatii sarufi. Hii haimaanishi kuwa hawajasoma Kiswahili lakini inaonyesha kuwa kuna maafikiano. Afisa wa polisi binafsi anazungumza kama washiriki wengine wa kundi hilo ili kupunguza mipaka baina yao, ingawa anajua kuwa anazungumza visivyo. Hii ni njia moja ambayo tunatumia kutambulisha kikundi hiki cha kijamii.

Gumperz (1971: 114) anasema kuwa:

> ……….makundi yote ya kijamii yanayojulikana huwa na lugha. Kinyume na ilivyo ishara zingine, mazungumzo, kwa njia ya kisarufi na mfumo wa kisemantiki, vyaweza kutumiwa kuashiria vifaa na dhana. Kwa wakati huo huo, kuhusiana kupitia kwa mazungumzo ni mchakato wa kijamii ambapo usemi huteuliwa kutegemea matarajio na mazoea.(TY)

Kwa mujibu wa maoni haya ya Gumperz ni kuwa kikundi cha kijamii huzungumza kwa namna fulani kutokana na mazoea ya kundi hilo. Kuvunja sarufi kwa maafisa wa polisi ni hali ya kuonyesha mazoea ya kikundi hiki. Hii inaonyesha kuwa pana maafikiano baina yao. Maafikiano haya yanadhihirika kwa maafisa wa polisi licha ya kuwa wanavunja sarufi. Kwa mfano

Mfano 13:

Afisa 1: Na ile mtu anasoma naye ni ile jamaa ya Nigeria.

Afisa 2: Ile jamaa yetu amejiunga na watu baya.

Afisa 3: Walienda kufunzwa halafu watakuja na hiyo pesa.

(Afisa 1: Na ule mtu wanasoma naye ni ule jamaa wa Nigeria)

(Afisa 2: Ule jamaa wetu amejiunga na watu wabaya.)

(Afisa 3: Walienda kufunzwa halafu watakuja na hizo pesa.)

Maafisa hawa watatu wa polisi wamevunja sarufi ya lugha ya Kiswahili. Katika mazungumzo haya maafisa wa polisi wanavunja sarufi ambayo ni wazi. Kusema *ile mtu* badala ya 'ule mtu' ni jambo ambalo ni kosa la wazi lakini wanazungumza hivi kama njia ya kuafikiana. Hali hii inaashiria umoja wao na kuonyesha kuwa wao ni kikundi ambacho kinaweza kutambuliwa.

### 3.4.0 KUKATIZIANA USEMI

Kukatiziana usemi ni hali ambapo mzungumzaji anazungumza kisha msikilizaji anaanza kuzungumza kabla hajakamilisha alilokuwa akilisema. Maafisa wa polisi wanapozungumza wenyewe hukatiziana usemi kwa sababu mbalimbali.

### 3.4.1 KUJIELEZA

Katika mazungumzo ya kawaida, kila mshiriki huchangia kwa linalozungumziwa. Hii ni kwa sababu hamna anayedhibiti mazungumzo. Wazungumzaji huwasilisha hisia zao moja kwa moja. Wazungumzaji wanapozungumza wasikilizaji huweza kuwa na haja ya kujieleza, kwa hivyo wao huwakatiza wenzao waliokuwa wakizungumza. Kwa mfano,

Mfano 14:

Afisa 1: Ile njaa niko nayo, hata niliamka asubuhi………….

Afisa 2: Wewe unakunywa pombe na hukulangi kisha……..

Afisa 1:Hapana, kwanza pombe nimeweka dash kabisa. Niko karibu na

mwezi mzima.

Afisa 2: Kwani ukikunywa pombe…………

Afisa 1: Nikikunywa pombe inaniripua bwana. Wewe hutaamini ni mimi.

(Dash – nimeacha)

Mazungumzo haya baina ya maafisa wa polisi yanadhihirisha kukatiziana usemi. Mazungumzo kuhusu hali ya maisha yanaruhusu hali ya kukatiziana usemi. Afisa 1 anakatizwa usemi na Afisa 2 ambaye anataka kumweleza mwenzake kuwa njaa yake inasababishwa na unywaji wa pombe bila kula. Afisa 1 naye anamkatiza mwenzake kwa nia ya kueleza kuwa yeye hatumii pombe tena. Afisa 1 angemwacha afisa 2 akamilishe usemi wake, hangejieleza na afisa 2 angechukulia kuwa pombe ndiyo inasababisha njaa.

Kukatiziana usemi ni njia moja inayodhihirisha maafikiano baina ya maafisa wa polisi. Hali hii husaidia mtu anapotaka kujieleza. Msikilizaji huweza kuwa na jambo ambalo anataka kulieleza kabla ya mzungumzaji kumaliza usemi wake. Afisa 1 hangesubiri Afisa 2 amalize kusema kuwa njaa yake inasababishwa na unywaji pombe. Afisa 1 anamkatiza Afisa 2 ili kumweleza kuwa yeye ameacha kunywa pombe.

### 3.4.2 KUBADILI MADA

Mazungumzo ya kawaida baina ya maafisa wa polisi husheheni mada tofautitofauti. Kila mzungumzaji hunuia kuanzisha mada yake ili iweze kuzungumziwa. Kutokana na kuwa kila mmoja anataka kueleza kuhusu jambo fulani, basi hali hii ya kukatiziana usemi haiwezi kuepukika. Kwa mfano,

Mfano 15:

Afisa 1: Walienda kufunzwa……………..

Afisa 2: Wacha wakubali hii kitu imetoka US, kama wanataka…………….

Afisa 3: Si maseneta wangeongea na president. Wakae chini........

Afisa 1: Unajua si eti Raila ndiye atafanya, ataincite tu watu.

(US – United States –Marekani)

(President – Rais)

(Ataincite – Atachochea)

Katika mazungumzo haya, afisa 1 alitaka wazungumzie mwenzao ambaye amejiunga na chuo kikuu. Afisa wa pili anamkatiza na kuanzisha mada kuhusu ajenda za mrengo wa upinzani za kutaka pawepo na mazungumzo baina yao na serikali. Afisa 3 anaanzisha mada nyingine kuhusu mazungumzo baina ya viongozi na anatoa maoni kuwa maseneta wazungumze na rais. Maafisa hawa watatu wa polisi wanakatiziana usemi ili kuanzisha mada nyingine tofauti na inayozungumziwa

Kubadili mada kunaenda sambamba na kukatiziana usemi. Mada zinazozungumziwa aghalabu huwa nyingi kutegemea idadi ya wazungumzaji. Mada hizi hata hivyo hazijadiliwi kwa kina kutokana na ukweli kuwa muda wa mazungumzo ya aina hii huwa mfupi kwa maafisa wa polisi ambao wanapaswa kuwa tayari kwani wanaweza kuitwa wakati wowote ili kwenda kuthibiti usalama, hasa panapotokea jambo la dharura. Mzungumzaji hutoa wazo lake kisha mwingine naye kutoa wazo tofauti ambalo ni tofauti na la mwenzake na hii husababisha kukatiziana usemi, hasa ikiwa wazungumzaji wanazungumzia mambo ya kawaida maishani. Katika mfano tuliotoa

hapo juu, kuna mada ya elimu na siasa. Mada hizi mbili zimezungumziwa kwa muda mfupi sana. Haya yanatokea kwa sababu mazungumzo ya kawaida hayathibitiwi kinyume na ikiwa mazungumzo yanahusu usalama. Maafisa wa polisi wanakatiziana usemi na hii inaonyesha kuwa kuna maafikiano kwa kuwa hamna anayelalamika kuwa mada yake haijashughulikiwa vilivyo. Mada mpya inapoanzishwa tu wote wanaanza kuizungumzia.

### 3.4.3 UREJESHI

Tunaitumia dhana ya urejeshi hapa kwa maana ya kukumbuka mambo yaliyotukia hapo awali. Maafisa wa polisi wanapozungumza huweza kukumbuka jambo fulani. Ili kuwasilisha jambo alilolikumbuka, washiriki katika mazungumzo hayo wanalazimika kukatiziana usemi. Kwa mfano,

Mfano 16:

Afisa 1: Mwandikie huyu hii……………

Afisa 2: Na ulimwona yule mtu nilikwambia?

Afisa 1: Hee, huyo hajui hawa watu wa chini ndio wanajua hii maneno. Watu hawa……….

Afisa 3: Na ni nani alikuwa hapa?

Afisa 1: Tanui.

Afisa 1 anaanza kuzungumza kuhusu mambo waliyopaswa kuandika, kisha Afisa 2 anakumbuka jambo walilokuwa wamelizungumzia awali. Afisa 2 anamkatiza mwenzake ili kuvuta nathari yake kwa nia ya kutaka kuelezwa kuhusu waliyokuwa wameyazungumzia. Afisa 3 naye kwa kutaka kuelezwa aliyekuwa katika sehemu ya kurekodi matukio awali anawakatiza wenzake.

Maafisa wa polisi wanapokuwa wakizungumza kuhusu mambo ya kawaida, yaani yasiyohusu usalama, ukatizaji usemi hudhihirika. Washiriki wa mazungumzo hayo huwa hawana nia mbaya na hakuna anayeudhika kwamba hajapewa muda naye azungumze.

Katika utafiti wetu, tuligundua kuwa maafisa wa polisi hufanya hivi bila hiari yao. Hii ni sifa mojawapo inayoonyesha maafikiano baina yao. Wanapokatiziana usemi, hawarejelei yale waliyokuwa wakiyazungumzia. Mada inapobadilika, wanaendelea nayo bila kurejelea ya awali.

Pratt (1977: 101) anasema kuwa katika mazungumzo ya kawaida ni vigumu kufuata kanuni za kusubiri mmoja amalize usemi wake. Anasema kuwa, kukatiziana usemi ni jambo la kawaida na kuwa ni muhimu katika aina hii ya mazungumzo. Maoni ya Pratt yanaonyesha kuwa katika mazungumzo ya kawaida hamna taratibu zinazofuatwa za kila mmoja kupewa wakati wake azungumze. Msikilizaji huhitajika kusema maoni yake bila kusubiri mwenzake amalize na hali hii husababisha kukatiziana usemi.

Tumeonyesha sababu ambazo huwafanya maafisa wa polisi kukatiziana usemi. Sababu hizi zinatokea kwa maafisa wa polisi na kwa sababu hii inadhihirika kuwa kuna maafikiano baina yao. Mbinu hii ya kukatiziana usemi husaidia kuhakikisha kuwa kila mshiriki aliye na jambo la kusema amelisema bila yeye kusubiri wenzake wamalize mazungumzo ambayo kwa kawaida hayaishi pasi na kukatizwa usemi.

Katika uchanganuzi wetu wa sajili ya maafisa wa polisi, tumeonyesha namna wao huwasiliana wenyewe. Tumeonyesha namna wanapunguza mipaka baina yao na kuwa washiriki wa kundi

moja ambalo linaweza kutambuliwa kutokana na matumizi yao ya lugha ya Kiswahili. Tumedhihirisha kuwa kuna maafikiano baina ya maafisa wa polisi kutokana na matumizi yao ya lugha ya Kiswahili.

Maafisa wa polisi hufanya kazi ambayo huwafanya kukutana na raia wa matabaka yote. Raia wengine hufika kituoni kuripoti jambo, wengine huwa wamefikishwa kama washukiwa na wengine huwa ni mashahidi. Maafisa wa polisi huwasiliana na hawa raia na huwaita wateja wao. Maafisa wa polisi wanapokuwa kituoni, muda wao mwingi hutumia kuwahudumia wateja wao. Hii ndio sababu tunahitaji nadharia inayofuata.

## SURA YA NNE

## VITENDO USEMI KATIKA SAJILI YA MAAFISA WA POLISI

### 4.0 UTANGULIZI

Katika sura ya tatu, tumeangazia matumizi ya lugha ya Kiswahili baina ya maafisa wa polisi wenyewe. Tumeonyesha matumizi ya msimbo pana na msimbo finyu. Pia, tumeonyesha kuwa kuna maafikiano baina ya kikundi hiki cha kijamii cha maafisa wa polisi kutokana na matumizi yao ya lugha.

Katika sura hii, tunazingatia nadharia ya vitendo usemi katika sajili ya maafisa wa polisi. Tunaangazia mazungumzo baina ya maafisa wa polisi na wateja wao wengine walioko kituoni.Tunafanya hivi kwa kujikita katika nadharia ya vitendo usemi.

### 4.1 NADHARIA YA VITENDO USEMI

Searle (1980: vii) anasema:

> Nadharia ya vitendo usemi huanza kwa chukulizi kuwa kipengee kidogo zaidi katika mazungumzo ya binadamu si sentensi au ishara zingine, lakini ni kutendeka kwa vitendo fulani kama vile: kutoa usemi, kuuliza maswali, kutoa amri, kufafanua, kueleza, kuomba radhi, kushukuru, kupongeza na kadhalika. Mzungumzaji hutenda mambo haya kwa kutoa sentensi. (TY).

Nadharia hii inachukulia usemi kama vitendo. Searle anaonyesha kuwa kila usemi unaotolewa na mwanadamu huwa ni kitendo fulani. Katika sajili ya maafisa wa polisi, mazungumzo baina yao

na wateja waliofika kituoni husheheni vitendo ambavyo vinaweza kubainika. Nadharia hii imetuwezesha kubainisha namna kani ya mazungumzo hupelekea kitendo fulani kutendeka.
Schiffrin (1994: 85) anaonyesha kuwa; katika mawasiliano, washiriki huwa hawazingatii tu hulka za kiisimu za usemi, lakini hutegemea zaidi uelewa wa asili ya hali ya kijumla. Hii huwezesha usemi kuwa na uamilifu fulani ambao huwezesha kitendo kutendeka kwa hali hizo za kijumla katika mazingira fulani. (TY).

Maoni ya Schiffrin yanaonyesha kuwa vitendo fulani hutendeka kutegemea na mazingira ya washiriki wa vitendo hivyo. Maafisa wa polisi wanapozungumza na washukiwa hali zao huwa tofauti na wakati ambapo wanazungumza na raia waliofika kuripoti jambo. Hii husababisha kutendeka kwa vitendo tofauti kutegemea na anayezungumziwa ni nani. Maafisa wa polisi wanapozungumza na washukiwa hulazimika kutumia toni tofauti na wanapozungumza na raia wanaofika kituoni kuripoti jambo.

Katika utafiti wetu, Searle na Austin wanaelezea nadharia ya vitendo usemi na hii imetusaidia kuchunguza sajili ya maafisa wa polisi kutokana na maana ya msemaji. Maana ya sentensi zinazotolewa, dhamira ya mzungumzaji, anachoelewa msikilizaji na pia kaida ambazo huongoza vipengele vya kiisimu (Searle 1969: 21). Kwa hivyo, nadharia hii itatuongoza kuangazia mazungumzo ambayo hupelekea kutendeka kwa vitendo fulani. Tumegawa kazi yetu katika vipera mbalimbali kutegemea na dhamira ya usemi unaotolewa.

### 4.1.1 KUTOA AMRI

Maafisa wa polisi wanapotoa amri hutaka kitendo fulani kitendeke. Amri hutolewa hasa kwa washukiwa waliofikishwa kituoni. Tunagawa sehemu hii katika vipera viwili:

### 4.1.2 KUTOA ONYO

Mazungumzo baina ya maafisa wa polisi na wateja wao huwa ya kutoa onyo hasa kwa washukiwa na mashahidi. Onyo hutolewa kwa wateja hasa ikiwa hamna ushirikiano baina yao na maafisa wa polisi. Maafisa wa polisi hutumia sauti ya kuonya kama njia ya kudhihirisha mamlaka yao. Kwa mfano,

Mfano 17:

Afisa: Wewe unajua huyu?

Shahidi: Ndio afande.

Afisa: Amesema kuna mtu aliingia na kuchukua laptop yake. Wewe ulikuwa hapo ofisini.

Shahidi: Afande unajua…….

Afisa: Eeeh, tusichezeane hapa. Ni uongee ukweli, ukinidanganya tu kidogo, nitakuweka ndani. Unasikia?

( Laptop – Kipakatalishi)

Mazungumzo haya ni baina ya afisa wa polisi na shahidi aliyeletwa na jamaa aliyeibiwa kipakatalishi kutoka ofisini. Shahidi alipoanza kusita afisa wa polisi alilazimika kutoa onyo kuwa anatakiwa kuzungumza ukweli. Maneno ya afisa "Ukinidanganya tu kidogo, nitakuweka ndani" yanadhihirisha onyo. Maneno haya yanakuwa na athari kwa shahidi. Hiki ni kitendo cha lokusheni ambacho kinapelekea kitendo kutendeka. Shahidi anaanza kuongea ukweli kuhusiana

na anachokijua. Kutokana na onyo lililotolewa na afisa wa polisi, shahidi anabadilika na kuanza kuzungumza anachokijua kuhusiana na wizi wa kipakatalishi.

Mfano wa pili ni baina ya msichana aliyefika kudai vitu vyake vilivyo kwenye kituo cha polisi. Msichana mwenzake aliyepatikana na vitu hivyo yuko kwenye seli.

Mfano 18:

Msichana: Mimi hiyo vitu ni yangu si yake. Funga yeye lakini mnipe mali yangu.

Afisa: Nimesema ondoka hapa au pia wewe nikuweke ndani.

Msichana: Kwani….

Afisa: Bado hujanisikia?

Maneno ya afisa wa polisi yanamfanya msichana kunywea na kuondoka kituoni pasi na kuzungumza zaidi.

Mifano hii miwili inatudhihirishia yale Searle (1975: 60) anasema ni vitendo usemi visivyo vya moja kwa moja. Hii ni hali ambapo kitendo kimoja cha ilokusheni hutendeka kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa nia ya kutenda kitendo kingine. Maneno ya maafisa wa polisi yaliwafanya shahidi na msichana kujirudi wenyewe na kisha kutenda kitendo fulani. Vitendo vya msichana na shahidi vimesababishwa na athari ya maneno ya maafisa wa polisi.

### 4.1.3 KUVUTA NATHARI

Maafisa wa polisi wakati mwingine hulazimika kutoa usemi ambao unaonyesha kuwa wanataka kusema jambo muhimu kwa mteja. Maneno yao huwa ya kuvuta nathari ya msikilizaji ili awe makini. Kwa mfano

Mfano 19:

Mshukiwa: Kwani nimefanya nini?

Afisa: Wee, hebu sikia kile mi ninasema. Unawekwa ndani kwa sababu ya robbery with violence. Si ulikuwa hapo? Utajitetea kortini kesho.

( Robbery with violence – wizi wa mabavu)

Afisa wa polisi anazungumza na mshukiwa ambaye anadai kuwa yeye ameletwa kituoni bila kosa. Mshukiwa anapinga vikali kuwa yeye hana kosa. Maneno ya afisa wa polisi "Wee, hebu sikia…." ni ya kuvuta nathari ya mshukiwa. Mshukiwa anakuwa makini kusikiza yale yanayosemwa na kwa wakati huo huo anaacha kupinga na kusikiza. Afisa wa polisi anapoanza kuzungumza kwa kutumia maneno ya kuvuta nathari, mshukiwa anakuwa makini na anaacha kupinga. Hii inaonyesha kuwa maneno ya afisa wa polisi yamesababisha kitendo kutokea.

Aina hii ya kutoa amri inazua taharuki kwa mshukiwa. Taharuki hii inamfanya aweze kuwa makini ili kusikia kinachosemwa. Taharuki hii inabadilisha hali ya mshukiwa. Kitendo kinachosababisha hali kubadilika kinatokana na usemi wa maafisa wa polisi.

## 4.2.0 MATUMIZI YA MASWALI

Sajili ya maafisa wa polisi huwa na uulizaji wa maswali. Wateja wanapofika kituoni kama washukiwa au waliofika kuripoti huulizwa maswali na maafisa wa polisi. Maswali ni muhimu katika sajili ya maafisa wa polisi kwa kuwa, ili waweze kunakili wanavyopaswa, ni sharti kuuliza maswali ili kupata ufahamu.

King'ati (2002: 91) anasema kuwa kuuliza maswali ni njia mojawapo ya kupitisha ujumbe wakati wa mahubiri. Katika sajili ya maafisa wa polisi, maswali husaidia katika kupata ujumbe wanaouhitaji. Maafisa wa polisi huuliza wateja wao maswali ili kupata kujulishwa kuhusu jambo fulani.

Katika sehemu hii, tunaangazia baadhi ya maswali yanayoulizwa na maafisa wa polisi na pia umuhimu wa maswali hayo. Tumegawa sehemu hii katika vijisehemu kutegemea na maswali yanayoulizwa.

### 4.2.1 UCHUNGUZI

Maafisa wa polisi huuliza maswali ambayo yatawaelekeza kupata ujumbe fulani. Maswali haya huwasaidia maafisa wa polisi kupata ukweli wa jambo fulani kabla hawajanakili yanayosemwa. Kwa mfano

Mfano 20:

Afisa: Ni nini hii?

Abiria: Ni maziwa napelekea watoto.

Afisa: Na hii gunia imebeba nini nzito hivi?

Abiria: Ni scrap.

(Scrap – vyuma vikuukuu)

Gari aina ya matatu ilifika kituoni kukaguliwa. Afisa wa trafiki alipofika panapowekwa mizigo, alipata mizigo aliyoishuku. Kibuyu lita tano kilikuwa kimetiwa ndani ya karatasi tatu za plastiki. Afisa wa trafiki alishuku kilichokuwemo ndani na ikambidi kuuliza maswali ambayo yangemwezesha kupata habari kamili kuhusiana na kilichokuwa kimebebwa.

Abiria naye alishangaa kwa nini mizigo yake inakaguliwa ilhali kulikuwepo na mizigo ya abiria wengine. Abiria alipoambiwa afungue gunia na kibuyu alianza kumuuliza afisa wa polisi maswali huku akifungua mizigo yake.

Mfano 21:

Abiria: Kwani afande unafikiri mimi nimebeba nini? Chang'aa na bomu?

Afisa: Mama, hii ni kwa sababu ya usalama wako na wakenya wengine.

Abiria kwa kutaka kujua sababu ya mizigo yake kukaguliwa, hasa baada ya kuambiwa aifungue, anamuuliza afisa wa polisi maswali. Maswali haya ni ya kutaka kujua hisia za afisa huyu wa polisi.

Maswali haya yanaweza kuchanganuliwa kiisimu kama vitendo usemi. Afisa wa polisi anapomuuliza abiria maswali, anamjibu. Naye abiria anapomuuliza afisa wa polisi swali, anamjibu. Maswali ya afisa wa polisi yenyewe ni vitendo usemi, kwa sababu, yanamfanya abiria ashuku kuwa afisa wa polisi anafikiria kuwa amebeba vitu haramu kama vile pombe na vilipuzi.

Maswali ya abiria pia yanamfanya afisa wa polisi aweze kumweleza abiria kwa upole sababu iliyopelekea mizigo hiyo kukaguliwa ilhali abiria wengine walikuwa na mizigo ila haikukaguliwa.

#### 4.2.2 KUHIMIZA MAZUNGUMZO

Maafisa wa polisi huweza kutumia maswali ili kumfanya mteja aendelee kuzungumza. Maswali ya aina hii aghalabu huulizwa waliofika kuripoti jambo. Afisa wa polisi anasikiza kwa makini bila kuzungumza ila labda mteja anaposita huuliza swali kwa nia ya kumfanya aendelee kuzungumza. Kwa mfano,

Mfano 22:

Afisa: Unakumbuka hiyo siku vizuri, si ndio? Basi nieleze ilivyokuwa.

Mteja: Niliingia kwa gari baada ya graduation, nikaketi mbele kwa dereva. Kushuka gari sikuwa na kibeti.

Afisa: Ilikuaje mpaka kibeti ikapotea?

Mteja: Mtu mwingine aliingia naye akaketi kando yangu. Alikuwa amevalia miwani na jaketi kubwa iliyofika hadi kwa miguu yangu.

Afisa: Halafu?

Mteja: Huyo mbaba alishuka mbele kidogo.

Maswali haya ya afisa wa polisi hayahitaji majibu ila yanamhimiza mteja aendelee kuzungumza. Maswali haya ni vitendo usemi kwa kuwa yanapoulizwa, mteja anaendelea kuzungumza.

### 4.2.3 UREJESHI

Maswali yanayoulizwa katika kijisehemu hiki ni ya kumfanya anayeulizwa akumbuke jambo fulani. Kwa mfano,

Mfano 23:

Afisa: Ulisema hiyo ID ilipotea lini?

Ruth: Siku ya Ijumaa.

Afisa: Ilipotelea wapi?

Ruth: Nilikuwa nimeiweka kwa mfuko wa jaketi lakini kufika nyumbani sikuipata.

Afisa: Nini ingine ilipotea?

Ruth: Hakuna ilikuwa peke yake mfukoni.

(ID- kitambulisho)

Maswali haya yanasababisha kutendeka kwa vitendo. Ruth anapoulizwa maswali, anakumbuka namna kitambulisho chake cha chuo kilipotea. Hivi ni vitendo usemi kwa kuwa Ruth analazimika kukumbuka matukio ya hiyo siku ambayo kitambulisho chake kilipotea.

### 4.3.0 NIA YA MZUNGUMZAJI

Huu ni usemaji ambao huonyesha kusudio la mzungumzaji. Namna wazungumzaji wanakusudia kutenda jambo fulani. Katika data yetu, nia inakuwa kama mahitimisho katika shughuli fulani. Mzungumzaji anatoa maelezo kuhusu jambo fulani akiwa na nia fulani.

Nia huwa na kani ambayo hujitokeza kwa mazungumzo baina ya maafisa wa polisi na wateja wao. Maafisa wa polisi huwa na nia ambayo huwafanya kuzungumza kwa namna fulani.

Washukiwa wakati mwingine hubishana na maafisa wa polisi. Maafisa wa polisi huwaeleza wanayonuia kutenda hatimaye kuwahusu. Baada ya kuelezwa na maafisa wa polisi, washukiwa hupatwa na hisia fulani. Hisia hizi hutokana na maneno ya maafisa wa polisi. kwa mfano,

Mfano 24:

Afisa: Yaani, ni kusema tena unadai pesa zaidi?

Mteja 1: Hata yeye amenitesa vya kutosha.

Afisa: Si ile siku mlimalizana tena unataka kuanza maneno ingine.

Mteja 2: Afande, wacha nitatafuta pesa nimpee.

Afisa: (kwa mteja 1) Hata wewe kuwa binadamu.

Mazungumzo haya yanalenga kuonyesha msimamo wa mteja 1 ambaye anataka alipwe pesa. Afisa wa polisi anaonyesha hulka ya mteja 1 ya kutokuwa na utu. Nia ya afisa wa polisi ni kuonyesha kuwa mteja 1 anakosea ila hataki kumwambia moja kwa moja asije akaonekana kama anayemtetea mteja 2.

Usemi wa afisa wa polisi unaonyesha hitimisho kuwa mteja 1 anapaswa kuwa na utu. Usemi huu unadhihirisha kitendo kwa kuwa unakuwa kama kichocheo cha kumfanya mteja 1 kubadili nia yake ya kutaka alipwe pesa nyingi.

Umuhimu wa nia katika sajili ya maafisa wa polisi ni kuonyesha namna maafisa wa polisi wanavyowafikiria wateja wao. Afisa anapomwambia mteja 1 kuwa anapaswa kuwa binadamu (kuwa na utu) anatuonyesha kuwa hana utu na ni muhimu kuwa nao. Usemi huu wa afisa wa

polisi unamfanya mteja 1 abadilishe kiwango cha pesa alizokuwa anaomba na kwa hivyo ni vitendo usemi.

Maafisa wa polisi wakati mwingine hulazimika kuwaeleza wateja wao ukweli wa mambo hata kama hautapokelewa vyema. Kwa mfano,

Mfano 25:

Mteja: Nimekuja kuwithdraw ile kesi.

Afisa: Wewe ulileta habari za uongo, si ndio?

Mteja: Hapana nimeamua tu kumsamehe.

Afisa: Kumbe hata wewe ulikuwa umemkata mkono. Kwa hivyo mtawekwa ndani nyinyi wote.

( kuwithdraw –kuondoa)

Wateja wote- aliyekuja kuondoa kesi na mshtakiwa walishtuka na hawakuridhishwa na uamuzi wa afisa wa polisi.Usemi wa afisa wa polisi unawaathiri wateja. Mteja alidhani kuwa ni rahisi kufutilia mbali kesi aliyoiwasilisha kituoni. Mteja na mshtakiwa wanatiwa kwenye seli. Nia ya afisa huyu wa polisi ni kuonyesha mamlaka yake. Mamlaka ambayo yanamfanya awatie wote ndani kwa sababu aliyeshtakiwa pia alikuwa amefika kumshtaki mwenzake.

Afisa wa polisi anatumia mamlaka yake. Usemi wake unaashiria matumizi ya mamlaka aliyo nayo. Mamlaka haya yanatosha kuwa kitendo usemi na kwa hivyo usemi huu una nia ya kuwasilisha ujumbe wa ukweli ambao wateja hawa hawakufurahishwa nao. Ukweli kuwa wangelala kwenye seli wakisubiri kufikishwa mahakamani.Wateja wanaghafilika na usemi wa

afisa wa polisi. usemi ambao unawaathiri wateja. Katika mfano huu tunapata kuona athari na jukumu la vitendo usemi.

Vitendo usemi vimetuwezesha kuchanganua maana na vitendo vya mazungumzo kiisimu.

Searle (1980: 292) anasema kuwa:

Katika kutenda vitendo usemi, kila mzungumzaji huwa na fikra fulani akilini, naye msikilizaji anajua kuwa mzungumzaji ana imani au matarajio fulani. Pili, kila kitendo usemi husababisha athari fulani na kwa hivyo hubadilisha hali ya uhusiano; mzungumzaji na msikilizaji wana haki ya kufikiria hali mpya ya yale wasiopaswa kutenda na pia kufikiria kuhusu wanachotakiwa kutenda kwa nia ya kuwasiliana na kudumisha uhusiano uliopo. (TY)

Maoni haya ya Searle yanaashiria kuwa mzungumzaji na msikilizaji wana uhusiano fulani ambao unadumishwa katika mazungumzo huku kila mmoja akiwa huru kufikiria anayopaswa kutenda. Katika sajili ya maafisa wa polisi, tumeonyesha athari zinazosababishwa na usemi wa maafisa wa polisi. Maafisa wa polisi hutoa usemi unaodhihirisha mamlaka yao. Uhusiano baina ya maafisa wa polisi na wateja ukidhihirika kutokana na mazungumzo yao.

Katika uchanganuzi wetu wa sajili ya maafisa wa polisi kwa kujikita katika lugha ya Kiswahili tumeonyesha namna maana ya usemi unaotolewa na maafisa wa polisi unavyowaathiri wateja. Tumeonyesha pia kuwa maafisa wa polisi huwauliza wateja maswali ili kuweza kuelezwa mambo ya kimsingi. Kani ya vitendo vya usemi wa maafisa wa polisi husaidia katika kuwashawishi wateja wao kubadili namna wanavyofikiri na kutenda ili kudumisha uhusiano uliopo baina yao.Udumishaji wa uhusiano uliopo baina ya maafisa wa polisi na wateja

hurahisisha kazi ya maafisa hawa. Utekelezaji wa majukumu yao unarahisishwa uhusiano uliopo unapodumishwa.

Vitendo usemi huwa na sifa ya kutambulika kutokana na kinachosemwa na kani ya ilokusheni. Kinachosemwa na kani ya ilokusheni huwa na uhusiano wa karibu. Ili kutaka kujua athari ya kitendo fulani, sharti kuangalia kinachosemwa. Kinachosemwa humwathiri msikilizaji kwa namna fulani kutegemea na hisia zinazoibushwa. Haya tumeyaonyesha katika mazungumzo baina ya maafisa wa polisi na wateja. Tumeonyesha namna wateja huathirika kutokana na usemi wa maafisa wa polisi. Athari hizi huashiria vitendo usemi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 UTANGULIZI

Sura hii ambayo ni ya mwisho katika utafiti huu imenuiwa kutoa muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu. Tumetathmini nadharia tete za utafiti wetu ili kubainisha kama zinaunga mkono au zinapinga matokeo ya utafiti wetu. Mwishowe tumetoa mapendekezo kwa watafiti wa baadaye.

## 5.1 MUHTASARI

Sajili ya maafisa wa polisi imedhihirisha uwepo wa matumizi ya msimbo pana na msimbo finyu. Msimbo pana hutumika wanapozungumzia mambo ya kawaida ya maisha ya kila siku kama vile siasa, elimu na kadhalika. Maafisa wa polisi huzungumzia mambo haya wanapokuwa mapumzikoni. Maafisa wa polisi hutumia msimbo pana ili kuwasilisha hisia zao. Mazungumzo haya hueleweka na kila mshiriki wa mazungumzo hayo.

Msimbo finyu hutumiwa wanapozungumzia mada zinazohusu usalama wa nchi. Matumizi ya msimbo finyu huwa yanasaidia katika kutenga makundi ambayo hayahusiani na usalama nchini. Maafisa wa polisi wamebuni sauti za irabu na konsonanti. Sauti hizi huwakilishwa na majina tofautitofauti. Jina moja husimamia sauti moja tu. Hii inaonyesha kuwa wao ndio watakaozielewa wanapozitumia.

Matumizi ya msimbo pana na msimbo finyu yamedhihirisha kuwa nadharia ya misimbo ya Bernstein inaakisi sajili ya maafisa wa polisi.

Maafisa wa polisi wanapowasiliana, huchanganya ndimi. Lugha ya Kiswahili hutawala mazungumzo yao huku wakichopeka maneno ya lugha ya Kiingereza au lugha zao za kwanza. Mazungumzo ya maafisa wa polisi husheheni kukatiziana usemi. Kukatiziana usemi husaidia katika kuhakikisha kuwa kila mshiriki aliye na jambo amelisema bila kusubiri wenzake wamalize usemi wao. Kuchanganya ndimi na kukatiziana usemi kunaonyesha kuwa pana maafikiano baina ya maafisa wa polisi. Maafikiano haya yanawatambulisha kama kikundi maalum cha kijamii.

Mazungumzo baina ya maafisa wa polisi na wateja wa ambao ni raia wanaofika kituoni yamedhihirisha kuwa maafisa wa polisi wana mamlaka. Haya yamedhihirika kutokana na usemi wa maafisa wa polisi ambao hupelekea kitendo fulani kutendeka. Usemi huu wa maafisa wa polisi huwa na athari fulani kwa wateja.

Wateja hulazimika kutenda kitendo fulani baada ya usemi wa maafisa wa polisi. Vitendo hivi hutokana na athari za usemi wa maafisa wa polisi. Athari hizi ndizo vitendo usemi. Kutokana na haya, ndiposa tunasema kuwa nadharia ya vitendo usemi inaafiki sajili ya maafisa wa polisi.

## 5.2 HITIMISHO

Tulitambua nadharia tete tatu kwa ajili ya utafiti huu. Nadharia tete yetu ya kwanza ilidai kuwa sajili ya maafisa wa polisi inahusishwa na matumizi ya msimbo, kuchanganya ndimi na sauti yao hudhihirisha mamlaka. Matokeo yanaonyesha kuwa maafisa wa polisi huchanganya ndimi, hutumia msimbo pana na msimbo finyu na pia hudhihirisha mamlaka yao wanapozungumza na wateja wao. Hivyo basi, nadharia tete hii ni kweli kabisa.

Nadharia tete ya pili ilidai kuwa sajili ya maafisa wa polisi ina uamilifu fulani katika utekelezaji wa majukumu yao. Katika uchanganuzi wetu, tumeonyesha kuwa maafisa wa polisi wanapozungumza na wateja wao hudhihirisha mamlaka na pia huwataka wateja kushirikiana nao ili kurahisisha kazi hasa wanapotoa amri. Nadharia tete hii basi ni kweli.

Matokeo ya uchanganuzi wa athari zinazotokana na sajili ya maafisa wa polisi yanakubaliana na nadharia tete ya tatu kwani maafisa wa polisi wanapozungumza na wateja hudhihirisha mamlaka. Matumizi haya ya mamlaka huwatia hofu wateja na kuwafanya kughairi nia yao ya awali. Athari za usemi wa maafisa wa polisi hupelekea kutokea kwa vitendo ambavyo kiisimu tumeviita vitendo usemi.

## 5.3 CHANGAMOTO ZA UTAFITI

Ni muhimu kutaja kuwa katika utafiti wetu tumekumbana na changamoto kadhaa. Haikuwa rahisi kukusanya data kutoka kwa maafisa wa polisi katika kituo cha polisi cha Central pekee yetu. Ilitulazimu kutafuta atakayetuongoza ambaye ni afisa wa polisi katika kituo hicho. Maafisa wa polisi walishuku uwepo wetu kituoni kila mara hasa kama kiongozi wetu alikuwa mbali, hii ilitulazimu kufika kituoni wakati ambapo yupo zamu.

Kituo cha polisi cha Central huwa na shughuli nyingi, maafisa wa polisi huingia na kutoka na muda wao wa mazungumzo huwa mfupi. Tulilazimika kurekodi mazungumzo yao kwa wakati tunaowapata na wakati mwingine tulirekodi mazungumzo ya dakika chache sana. Hatukuwa na uwezo wa kuwazuia au kuwafanya waendelee na mazungumzo kwa kuwa hawakujua kama tulikuwa tunafanya utafiti.

Katika utafiti wetu, tuliweza kupata idadi ya maafisa wa polisi tulioazimia kurekodi kutoka kila kitengo ila ilitubidi kubana habari zingine kwa ajili ya usalama hasa mazungumzo baina ya maafisa wa polisi wa upelelezi. Gharama ya utafiti vilevile ilikuwa juu. Hata hivyo, tulijizatiti na kufanikiwa kumaliza utafiti wetu kwa wakati ufaao.

## 5.4 MAPENDEKEZO

Katika utafiti huu, tulibanwa kwa upeo na mipaka yetu kwani kuna mambo mengi ya kutafitiwa katika eneo hili la sajili ya maafisa wa polisi na ambayo tulilazimika kuyaacha nje. Kutokana na utafiti huu tumegundua kuwa sajili ya maafisa wa polisi ina uamilifu na athari kwa wao wenyewe na pia wateja wao na kwa hivyo tungependekeza:

Katika utafiti wetu, tulijikita katika kituo cha polisi ambako maafisa wa polisi hutangamana na wateja wanaofika kwa sababu tofautitofauti, tungependekeza watafiti wachunguze maafisa wa polisi wa gereza ambao hutangamana na wafungwa waliohukumiwa kifungo fulani na washukiwa wanaosubiri kuhukumiwa. Hii itawezesha kupata sajili ya maafisa wa polisi ambao hutangamana na watu mahsusi.

Mbinu yetu ya utafiti ilikuwa ni kurekodi mazungumzo ya maafisa wa polisi. Hii ilituwezesha kupata data tuliyoihitaji katika uhalisia wake. Hata hivyo kuna mambo mengi ambayo hatukujua maana yake na pia sababu zinazowafanya wao kuzungumza kwa njia fulani. Kwa sababu hii, tungependekeza watafiti watumie njia tofauti za utafiti kama mahojiano ili kupata maoni mbalimbali kutoka kwa maafisa wa polisi.

Utafiti wetu ulifanyika katika kituo cha polisi cha Central mjini Nairobi, kituo ambacho ni kikubwa. Tungependekeza utafiti ufanywe katika vituo vingine vya polisi nchini Kenya na kulinganisha matokeo hayo.

Utafiti wetu haukuonyesha tofauti ya sajili ya maafisa wa polisi walio na viwango tofauti vya elimu. Hivyo basi tafiti zifanywe kubainisha iwapo maafisa wa polisi waliosoma na kupata shahada za digrii na pengine uzamili huzungumza kama wenzao kwa kuchanganya ndimi na kuvunja sarufi.

Sisi tulijikita katika mazungumzo ya maafisa wa polisi bila kuzingatia umri, tunapendekeza utafiti ufanywe ili kubaini matumizi ya lugha ya maafisa wa polisi walio na umri mkubwa na wale walio vijana. Kwa sababu, vijana na wazee  wamepitia mafunzo katika nyakati tofauti.

## MAREJELEO


Austin, J. L. (1962) *How to do things with word.* New York: Oxford University Press.

Bernstein, B. (1971) *Class, Codes and Control*. London: Routledge and Kegan Paul publishers.

___________(1972b) *Social class, language and socialization* in Giglioli. London: Routledge and Kegan Paul Publishers.

Fairclough, N. (1989) *Language and Power.* London: Longman.

Fishman, A.J.(1968) *Reading in the Sociology of Language*. Hague: Mouton and Co.N.V P Publishers.

Giles, H. (1975) *Speech Style and Social Evaluation*. London: Academic Press INC.

Gumperz, J. (1971) *Language in Social Groups*. California: Stanford University Press, Stanford.

Gumperz, J.(1972) 'Introduction' in J.J Gumperz and D. Hymes (eds). *Directions in Sociolinguistic:Ethnography of Communication*. New York: Holt, Rinchart and Wiston Inc.

Habwe, J. H. (1999) *Discourse Analysis of Swahili Political speeches*. PhD Thesis (unpublished), University of Nairobi.

Habwe n.w (2010) *Darubini ya Isimujamii*. Nairobi: Phoenix publishers.

Hudson, R .A (1980) Sociolinguistics, Cambridge: Cambridge University Press.

Iribemwangi, P. I. na A. Mukhwana, (2011) *Isimujamii*, Nairobi: Focus Publishers.

Kingati, J. B. (2002) *Swahili Homilies*. M.A Thesis (unpublished), University of Nairobi.

Leech M. na C.S. Silva,(2006) *Language Proficiency and Police Officers' Lie Detection Perfomance*. Available from URL. http;//www.atimes.com

Mang'eni, N. L. (2008) *An Analysis of Political Language In Kenya: A Pragmatic Analysis ofuse 'change' and 'majimbo' as Concepts During the 2007 General Elections*. M. A Thesis (unpublished), University of Nairobi.

Mekacha, D. K. (2011) *Isimujamii:Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. Dar es salaam: Osaka University of Foreign Studies.

Michira, J. N. (1993) *Uchanganuzi wa Kimtindo wa Lugha ya Wachuuzi na Lugha ya Matangazoya Biashara Redioni*. M.A Thesis (unpublished), University of Nairobi.

Mugenda, O. na A. Mugenda, (2003) *Research Methods:Quantitative and QualitativeApproaches*. Nairobi: ACTS Press.

Mukhwana, A. (1990) *Siasa na Uimarikaji wa Kiswahili Kenya*. M.A Thesis (unpublished), University of Nairobi.

____________ (2008) *Language Attitudes in Urban Kenya. A Case Study of Nairobi, Kisumu and Mombasa*. PhD Thesis (unpublished), University of Nairobi.

Njenga, P.G. (2008) *English-Kiswahili code-switching in Easy FM: The Markedness Model*. M.A Thesis (unpublished) University of Nairobi.

Pratt, M. L. (1977) *Toward a Speech Act Theory of Literary Discourse*. London: Indiana University Press Bloomington.

Pride, J. B.(1971) *The Social Meaning oa Language*. New York: Oxford University Press.

Schiffrin, D.(1994) *Approaches to Discourse*. Cambridge: Blackwell Publishers.

Searle, J. R. (1975) '*Indirect speech Acts'*, in P. Cole and J. Morgan, sytanx and semantics 3. New York: Academic Press.

___________(1980) *Speech Act Theory and Pragmatics*. London: D. Reidel Publishing Company.

Spolsky, B. (1998) *Sociolinguistics*. New York: Oxford University Press.

Stockwell, P. (2002) *Sociolinguistics*. London: Routledge.

Thomas, L. na S. Wareing, (1999) *Language, Society and Power*. London: Routledge.

Trudgill, P. (2000) *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society*. London: Penguin Books.

Vahid, D. H. n.w (2008) *Analysis Of Power and Threat Manifestation In TheDiscourse of TrafficPoliceOfficers*. https://www.equinoxpub.com/journals/index.php//Jsll/article/view/1005.

Wardhaugh, R. (1986) *An Introduction to Sociolinguistics*. oxford: Blackwell Publishing.

Whitely, W. H. (1974) *Language in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

## DATA YA UCHANGANUZI

Data hii ilikusanywa kutoka kwa kituo cha polisi cha Central. Maandishi haya yamehifadhiwa katika hali yake halisi na hakuna juhudi zozote zimefanywa za kurekebisha makosa ya tahajia au ya kisarufi.

1. Afisa wa polisi: Nikusaidiaje?

   Ruth: Nimekujia abstract.

   Afisa wa polisi: Enda huko canteen uwaambie wakupatie ndio ukuje nayo hapa.

   Ruth: Sawa.

2. Afisa wa polisi: Umepata?

   Ruth: Wameniambia mwenye anapeana hayuko. Sasa utanisaidiaje afisa?

   Afisa wa polisi: Hii yangu nimenunua pesa nyingi sana. Sitaki kupeana tu hivi hivi tu.

   Ruth: Nitaigharamia

   Afisa wa polisi: Sawa chukua enda room 17 ujaziwe ndio unione.

   Ruth: Nashukuru.

3. Ruth: Naomba unijazie hii abstract.

   Afisa wa polisi: Umepoteza nini?

   Ruth: School ID.

   Afisa wa polisi: Unasomea hapa Nairobi?

   Ruth: Ndio afande.

   Afisa wa polisi: Wapi barua ya dean of faculty ya kuonyesha unasomea huko?

   Ruth: Afande sikujua eti ni sharti uwe na barua.

Afisa wa polisi: Nitakusaaidia lakini ulipe fare yangu ya kwenda nyumbani.

Ruth: Ngapi afande?

Afisa wa polisi: Si unajua leo ni weekend na umekuja jioni sana, we leta kitu.

Ruth: Sawa nashukuru.

4. Afisa 1: Ako directly below chief security officer.

   Afisa 2: One?

   Afisa 1: Si ndio, ile inspector of police one.

   Afisa 2: Na hao watu sasa……….

   Afisa 1: Hao ndio wanakaribia hapo kabisa.

5. Afisa 1: Hii kitu black hapana weka hapa.

   Afisa 2: Si yeye amekula.

   Afisa 3: Bakishia yeye. Haijafika? Mbona huendi kwake?

   Afisa 1: Omera, leta hii…………..

   Afisa 3: Anashangaa, wewe nani amekula?

   Afisa 2: Mzee.

   Afisa 1: Shika changia yeye.

   Afisa 2: Hiyo utachanga pole pole.

   Afisa 1: Shika hii weka hapo, haijaandikwa jina lako.

6. Afisa 1: We toa kila kitu kwa mfuko wekelea hapa.

   Mshukiwa: Sawa.

   Afisa 1:Hii ni pesa ngapi?

   Mshukiwa: Mimi sina pesa mingi.

   Afisa 1: Andikia yeye mia mbili.

   Afisa 2: Si ulete basi, sitaki kuandika kama sijaona hiyo pesa. Naandika nikiwa nayo.

   Afisa 1: Unaona wewe, nani amekupatia hii pesa?

   Afisa 2: Ni huyu, ninaandikia.

   Afisa 1: Huyu hajui hawa watu wa chini ndio wanajua hii maneno. Watu hawa walikuwa wanatengeneza biashara sijui wapi sijui wapi. Kumbe………..

   Afisa 3: Nani alikuwa hapa?

   Afisa 1: Tanui.

   Mshukiwa: Afisa si nilikuwa nimeongea na wee?

   Afisa 3: Ati tuliongea na wewe, saa ngapi?

7. Afisa: We unatakaje hapa?

   Mteja: Nimekuja kumtoa Joni.

   Afisa: Alileta saa ngapi?

   Mteja: Saa nane hivi.

   Afisa: Aah huyo ni wa kanjo. Ingia hapa ongea na huyo.

8. Afisa 1: Unajua hii jamaa inaitwa Markomen?

   Afisa 2: Murkomen anasema tu.

Afisa 1: Yenyewe ni ngumu, 2017 hata kama tunasema ni politics.

Afisa 3: Ukweli hatuogopi Raila.

Afisa 1: Lakini hapana unaona 2017, Raila atachukua kama ile Kibaki alichukua wakati alikuwa ametoka hapo. Sikudanganyi Raila atachukua.

Afisa 2: Na akichukua atasafisha ile ghasia yote imetokea kwa hii nchi.

Afisa 1: Unajua huyu mzee, si pekee yake.

Afisa 3: Si ati atasafisha, unajua hii serikali ya vijana si mbaya. Hii serikali ya vijana ni kama hata wamechagua tu kabila yao, maaskari siku hizi hatukuli.

Afisa 1: Unaona kitu moja unajua Uhuru alifanya kitu mzuri sana kama ni pesa utakuta wanatafuta na hawataki kufail watu hiyo ndio kitu moja ninaona.

Afisa 2: Lakini kwa sababu wanajua starehe ya watu ni kwa power, ziko power wanaexercise kwa power za………………

Afisa 1: Hiyo ni automatic.

Afisa 3: Hata Uhuru alisema.

Afisa 2: Unakataza watu wasi……………

Afisa 3: Wee sikia nikueleze u've talked about your mind. Kitu mi naweza sema hata kama ni nani, hii serikali hataiweza.

Afisa 1: Kwa nini?

Afisa 3: Hii katiba aah yenyewe ni mbaya.

Afisa 1: Hata Kibaki alikuwa na governors, alikuwa na same people wenye…………

Afisa 2: Alikuwa na serikali ingine ya county.

Afisa 3: Ndio, lakini hawa wamejaribu na wanafanya kazi lakini hii Kenya ingekuwa inaendeshwa na America waah.

Afisa 1: Tusidanganyane.

Afisa 3: Sawa lakini mimi nilienda wakati ya vurugu na nikakaa Tana Delta. Wakati ile kitu ilikuwa political na siku hiyo nilikaa Witu. Watu wanakuja mpaka unashangaa.

Afisa 2: Si tuliandika, si tuliokota hiyo makaratasi yote mpaka hata wakikuyu walitoka Malindi wakasema hii kitu ni ya zamani si ya saa hii.

Afisa 3: Waliandikiwa barua, aa karatasi wakaambiwa watoke Mombasa yote, Malindi yote, waende…………..

9. Afisa akizungumza kwa radio ya maafisa wa polisi.

Shika ile motocycles wale wanatuleteanga shida na wale watu wa Mututho washikwe.

Hata huko ukipatrol Eastern bypass na ukuje mpaka aaah …………. Kwa kuwa wewe unajua dangerous areas. Hiyo area ya Pipeline teremka chini ukisaidiana na yule mtu ya Kware and let them touch Mombasa road.

Ukuje Umoja 3 upande ya Kangundo road over. Kindly madam you can inform the power personel there is a live wire, a live wire which has fallen down within Umoja 3, Umoja 3.

Ooh roja habari ya saa hii, aah welcome back. Patrol kila mahali hapo because of world cup over. Every patron to be searched. Mututho time wacha watu washikwe hatutaki shida roja.

10. Afisa 1: Kwa serikali, ako na afya kuliko askari bwana, halafu.

Afisa 2: Ako na chapaa.

Afisa 1: Ilileta shida na…………..

Afisa 3: Na ile shamba yake……….na wamepewa shamba.

Afisa 1: Wewe buldoza wakati sisi tulikucha kwa hii kazi, hakuna kitu kama hiyo ilikuwa inaendelea.

Afisa 3: Wewe ndio mjinga hapa 1987, 87 tulikuwa tunaunda pesa.

Afisa 1: Na sasa………..

Afisa 2: Hii ya Naivasha………..

Afisa 3: Iko wapi?

Afisa 2: Kama unaingia tu Naivasha.

Afisa 1: Ya Naivasha sasa tulikuwa tunapata live.

Afisa 3: Si eti unaonekana, unaingia ndani na kupata unapata pesa nyingi.

Afisa 2: Siku hizi unajifanya na ukae ukiangalia tu kando ukipokea.

11. Afisa 1: Tulikuwa tunasumbuliwa, na unajua tulikuwa watu wangapi, 30 only.

Afisa 2: Sasa hata………………

Afisa 3: Sasa hii ya pili niliingia nayo hata hakuniangalia macho direct.

Afisa 4: Kwanza wewe ndio ulikuwa mtu wa kwanza.

Afisa 1: Yeye ndiye alikuwa pale bado?

Afisa 3: Bado ni yeye, nyumbani ni wapi?

Afisa 2: Eeh nyumbani ni wapi? Nikaeleza yeye. Eeeh county yako ni gani? Nikamwambia, na constituency? Nikamwambia akasema ni sawa.

Afisa 3: Hiyo sasa ni nini?

Afisa 2: Eeh akasema sawa, nikauliza Samoei kuna swali amekuuliza?

Afisa 1: Hata hii ya pili ni kama amerudi chini.

Afisa 2: Samoei aliniuliza, what is a nation? Nikamwambia.

Afisa 1 na 3: Mmmh eti?

Afisa 2: Nikamudefainia. Halafu ananiuliza ulisomea nini university? Nikamwambia. Akaniuliza now what is tautology? Nikamwambia halafu yeye akaniuliza what is the difference? Nikamdifferentiatia. Lakini akasema aah hiyo………..

Afisa 3: Hiyo bado.

Afisa 2: Hiyo bado. Sawa nikarudi tena kwa Maingi. Maingi akaniuliza, who is the chairman ya parliamentary security committee? Nikamwambia Asman Kamama. Nikamwambia honourable Kama….. Kamama.

Afisa 3: Mmmh!

Afisa 2: Halafu akaniuliza from which constituency? Sikuwa nakumbuka.

Afisa 4: Ni Pokot hiyo jamaa.

Afisa 1: Eeh.

Afisa 2: Huwezi sema hujui. Nikasema am not sure. Akaniuliza what are you not sure of? Ungesema hiyo yenye hauko sure ndio ungojee for correction. Nikamwambia I don’t know. Akaniambia okay you can follow up. Yaani ikaishia hapo.

12. Afisa 1: Jambo afande?

Afande: How do you do? We have to wait. Okay?

Afisa 2: Not yet!

Afande: Yes, because kuna hawa new recruits.

Afisa 2: Unajua kuna wengine hawajapata mshahara bado.

Afande: Correct. Ndio hayo. Ilikuwa wafunge jana saa tisa usiku. Akaniambia ataniambia juu ametoka kazi late sana saa saba usiku. Saa hii ndio alikuwa aingie kitu saa nne job. I can even call him once again.

Afisa 1: Yeye hukuupdate hapa kila wakati.